epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii

# Nipashe

Alhamisi Januari 9, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581916

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

Nipashe digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710

LIKE & FOLLOW US



Mgombea nafasi ya Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Odero Charles Odero (kushoto), akirejesha fomu ya kugombea nafasi hiyo katika ofisi ya chama Kanda ya Kaskazini. Kulia ni Leha Mushi Ofisa wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbowe na Tundu Lissu wageuziwa kibao

• **Mgombea** uenyekiti adai wamevunja Katiba... *Ukurasa 2*

## Aliyemvalia mchumba sare za JWTZ, jela miezi 6 UK. 5

UKURASA WA 3

**ACT** Wazalendo yaja na tathmini ya 2024 iliyojaa lawama, utekaji

UKURASA WA 7

**Adaiwa** kumuua mwanawe kisa kutomrudishia chenji ya 9,000/- kununua chapati



UKURASA WA 8

**TEHAMA** yapunguza msongamano wa mahabusu gerezani

# Rais Samia atangaza marufuku divisheni IV na sifuri, zamkera UK. 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Misufini iliyoko Bumbwini, Zanzibar baada ya kuifungua jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** SIMBA: TUNAKWENDA KUFUNGA HESABU UK.24 **MAONI,** UK.6



Mkazi wa jijini Dar es Salaam akisambaza udongo kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho jana, ili kuziba mashimo yaliyopo kituoni hapo yanayosababisha usumbufu kwa madereva. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Rais Samia atangaza marufuku divisheni IV na sifuri, zamkera

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameeleza kukerwa na matokeo mabaya ya elimu kwa wanafunzi wa shule za Zanzibar kwa madaraja ya sifuri na la nne na kusema hataki tena kuona hali hiyo ikiendelea.

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa Shule ya Sekondari Bumbwini Misufuni, Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwa sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi, Rais Samia alisema hakuna sababu ya Zanzibar kuwa na matokeo mabaya kwa sababu serikali inajitahidi kuboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga shule za kisasa.

Alisema miongoni mwa malengo ya Mapinduzi ni kuwaletea maendeleo wananchi na waasisi wa Mapinduzi hayo waliweka misingi mizuri na waliendana na malengo ya dini kwa kuhakikisha jambo la kwanza ni elimu na kutoa elimu bure.

Rais Samia alisema alianza kusoma darasa la kwanza mwaka 1965 baada ya Mapinduzi na alisoma katika Shule ya Msingi Kitogani iliyojengwa kwa makuti, maarufu ikiitwa Mabanda ya Mbuzi.

Baada ya Mapinduzi, alisema viongozi awamu kwa awamu waliboresha misingi ya elimu kwa kujenga shule nzuri.

Alisema zamani Zanzibar ilikuwa nyuma kiufaulu kwa sababu hakukuwa na maabara za kisasa, hivyo kwa sasa lazima wanafunzi wasome kwa bidii na kufaulu.

Kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar, alisema kulikuwa na shule 92 zikiwamo sekondari tano na chekechea moja pekee lakini hivi sasa kuna shule 1,308.

"Malengo ya Mapinduzi ni kustawisha hali za wananchi wake, zikiwamo kielimu na kiafya," alisema.

Rais Samia alisema maono ya serikali ni kuzalisha wataalamu wenye ujuzi ili kusaidia taifa lao na kubainisha kuwa kazi nzuri haijafanyika kuzalisha wataalamu katika sekta ya utalii na pengine kulichangiwa na utamaduni wa kuonekana kuwa kazi hizo hazina staha ndiyo maana Wazanzibari ni wachache katika ajira kwenye eneo hilo.

Aliwataka wazazi kuhakikisha watoto wanasoma kwa bidii ingawa serikali inabeba msaada wa kutoa elimu bure, hivyo panapohitajika wazazi kutosita kusaidia.

Pia aliwataka makandarasi na washauri elekezi wa majengo kufanya kazi kwa uadilifu ili majengo yanayoendelea kujengwa yawe bora na ya kiwango ili yadumu kwa muda mrefu.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa, alisema serikali zote mbili zimewekeza kwa kiasi kikubwa kuboresha miundombinu, maslahi ya walimu na vitendea kazi katika sekta ya elimu.

Alisema hali hiyo imesaidia kupata mafanikio katika sekta hiyo ikiwamo kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa.

Waziri Lela alisema hayo ni matunda ya Mapinduzi na wanafunzi wanasoma katika mazingira bora na ni dhamira ya serikali kutoa elimu bora inayokwenda na wakati ulimwenguni.

Alisema katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Dk. Mwinyi, Wizara ya Elimu imejenga shule 35 za ghorofa na 28 ziko katika hatua za ujenzi, ukarabati wa shule zote chakavu, kukamilisha ujenzi wa madarasa yaliyoanzishwa na wananchi ili wanafunzi kusoma katika mazingira rafiki.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Abdallah Khamis Said, alisema ujenzi wa shule hiyo ni juhudi na serikali kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani na ulianza Septemba, 2023 na kukamilika mwishoni wa mwaka 2024.

Alisema thamani ya ujenzi huo ni Sh. bilioni 6.1 na ni ya ghorofa tatu na ina madarasa 40, maktaba, maabara, mabweni ya wanafunzi, nyumba za walimu na ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,841 kwa wakati mmoja.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zahro Mattar, alisema kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar, mkoa huo ulikuwa na shule zisizozidi tatu lakini hivi sasa una shule 152 kwa ngazi mbalimbali kuanzia maandalizi, msingi na sekondari.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Mbowe na Lissu wageuziwa kibao uchaguzi wa CHADEMA

**Na Vitus Audax,** DODOMA

WAKATI minyukano ikiendelea kati ya ngome ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na Makamu wake, Tundu Lissu, mgombea wa tatu wa nafasi ya uenyekiti wa chama taifa, Charles Odero amesema kinachoendelea ni ukiukwaji wa Katiba ya chama hicho.

Miongoni mwa vitu alivyodai Odero kuwa ni ukiukwaji matakwa ya kikatiba ni wagombea hao kuwa na wenza katika uchaguzi huo, makundi, kuunda timu, kuanza kampeni kabla ya muda pamoja na kutangaza kura kinyume cha utaratibu.

Odero ambaye tayari amechukua fomu kuwania kiti hicho, alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati akizungumza na Nipashe iliyotaka kujua kilicho nyuma ya ukimya wake baada ya kuchukua fomu licha ya wenzake kuonekana mara kwa mara hadharani.

Alisema Katiba ya chama hicho imeweka wazi nafasi zinazotakiwa kuwaniwa kuwa ni pamoja na Mwenyekiti Taifa, Makamu Mwenyekiti Bara na Zanzibar pamoja na wajumbe wa Kamati Kuu ambao wamegawanyika katika makundi matatu.

"Makundi hayo ni ya wanawake, wenye ulemavu pamoja na kundi mchanganyiko lakini hawa wenzangu wamekwenda mbali zaidi wamekuwa na kundi la mgombea na mgombea mwenza ambalo katiba ya chama haitambui hilo," alidai.

Odero alitaja jambo lingine analoona wagombea wenzake wanakiuka Katiba ya chama chao ni kutengeneza mtandao, akitolea mfano mtandao unaomuunga mkono Lissu pamoja na mtandao wa Mbowe.

"Si kwamba Katiba haijatoa mwanga kuhusu makundi, lakini katika uchaguzi huu imebainisha kuwa kila mgombea anatakiwa kugombea kama yeye na wala si kutengeneza makundi wala mtandao wa kuweza kupata uongozi," alisema Odero.

Aidha alitaja ukiukwaji mwingine wa Katiba ya chama chao ni baadhi ya wajumbe kutangaza wazi kura zao kupitia vyombo vya habari ilhali kura katika uchaguzi huo ni siri.

"Tumeona kwenye mikoa watu wanajitokeza wanasema 'sisi kura yetu ni kwa fulani', suala hili si sahihi kikatiba na kwa mujibu wa taratibu za kichama hazijaruhusu kampeni, lakini kinachoendelea kinaonesha ni kwa namna gani wananadiana," alisema Odero.

Alisema kuwa katika uchaguzi huo kila mmoja ana nafasi yake na akiipata atatakiwa kuitumikia kama yeye na wala si kwa msaada wa msaidizi wake kwa kuwa Katiba imebainisha kila nafasi na majukumu ya mhusika na wote watakutana katika Kamati Kuu.

Kuhusu Lissu kudaiwa kukichafua chama hicho kupitia tuhuma za rushwa dhidi ya baadhi ya viongozi, Odero alisema Katiba haijamzuia mtu yeyote kutoka nje na kueleza maoni yake.

Hata hivyo, Odero alisema licha ya Lissu kuwa mwanasheria na kiongozi katika chama hicho, anatakiwa kufuata njia sahihi za kiuongozi kuwasilisha jambo hilo ikiwa ni pamoja na kulifikisha kwenye uongozi pamoja na taasisi za serikali ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ili kama kuna wahusika wachukuliwe hatua za kisheria na si kuishia kuongea kwenye majukwaa.

Alisema kuwa katika mambo yanayohusiana na rushwa kwa mujibu wa Katiba ya chama hicho, mhusika anaweza kupewa onyo, kuvuliwa uongozi na hata kufukuzwa uanachama.

Kuhusu sababu ya yeye kugombea nafasi hiyo, Odero alijitambulisha kuwa "ni sura mpya ndani ya chama", anahitaji kuwaleta wana- CHADEMA pamoja na kuwa wamoja kueleka katika Uchaguzi Mkuu na ujenzi wa chama hicho.

"Nitawaweka pamoja wanachama wote, umma wa watanzania pamoja na viongozi wa chama chetu kuelekea katika mchezo pekee ambao kwetu mpinzani mkubwa ni CCM (Chama Cha Mapinduzi)," alisema Odero.

Alisema viongozi hao wanaochuana wameongoza kwa muda mrefu, hivyo ni wakati wa kuachia nafasi kwa sura mpya na fikra mpya ili kupeleka chama hicho mbali zaidi.

"Lissu na Mbowe wamekuwa kwenye uongozi wa chama hiki kwa zaidi ya miaka 24 sasa, sidhani kama wana fikra na maono mapya ambayo yatakayokifanya chama kuwa kipya, hivyo chama kinamhitaji Odero kwa ajili ya mageuzi," alisema Odero.

Kwa mujibu wa kanuni za kuendesha kampeni za ndani ya chama hicho, kanuni ya 2.0 (i-vii), ni kosa kwa mgombea au wakala kufanya kampeni kabla ya muda, kufanya kampeni chafu kwa kukashfu wagombea wengine kupitia njia mbalimbali za mawasiliano, kuhusisha ukanda, udini, ukabila au ubaguzi wa aina yoyote ile.

Vilevile, kanuni hizo pia zinaelekeza kuzingatiwa kwa masharti yaliyoainishwa katika mwongozo dhidi ya rushwa pamoja na kutokufanya kampeni kwa kujinasibu na kiongozi yeyote wa kitaifa, wilaya au kiongozi yeyote wa kuchaguliwa iwe kwa mazuri au mabaya.

Kifungu cha 3.0(i-v) kinaainisha adhabu dhidi ya ukiukwaji kanuni hizo kuwa ni pamoja na mhusika kupewa onyo, kupewa onyo kali au kuondolewa katika mchakato wa uchaguzi iwapo itathibitika kuwa mgombea amekiuka utaratibu wa kampeni kwa mujibu wa mwongozo huo.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam juzi, Katibu Mkuu wa CHADEMA hicho, John Mnyika aliwaonya wanachama, wagombea na mawakala wao dhidi ya ukiukwaji sheria na miongozo ya chama, akidokeza kuwa moja ya adhabu ni kuondolewa kwenye mchakato wa uchaguzi.

**HABARI KITAIFA**



Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert, akizungumza katika mafunzo ya jinsi ya kutembelea familia zenye watoto walio na ulemavu wa akili mjini Tabora jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT Wazalendo yaja na tathmini ya 2024 iliyojaa lawama, utekaji

**Na Restuta James**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetoa tathmini ya mwaka 2024, kikikumbusha matukio 12 ya kupotea kwa raia, huku kikijinasibu kusimamia mambo matano mwaka huu.

Aidha, kimeita vyama vingine vya upinzani kushirikiana ili kuweka mikakati ya kukiondoa Chama Cha Mapinduzi (CCM) madarakani kwenye Uchaguzi Mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Waziri Mkuu Kivuli wa chama hicho, Isihaka Mchinjita, alisema matukio ya kupotea kwa watu, yaliwapitisha wananchi kwenye mateso makubwa.

Mchinjita alisema, matukio ya kutekwa na kuuawa kwa aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ali Kibao, kuwa miongoni mwa matukio yaliyowaumiza wananchi.

Alitaja watu wanaodaiwa kutoweka kuanzia Januari Mosi, mwaka jana, kuwa ni William Herman, David Lema, Yonzo Shimbi, Lilenga Isaya, Simoni Nairiam, Edgar Mwakalebela, Abdul Nondo, Deusdedit Soka, Frank Mbise, Jacob Mlay na Shadrack Chaula.

"Licha ya matukio yote haya ya wazi kabisa, Jeshi la Polisi halijatoa taarifa yoyote ya kina kuhusu matukio haya licha ya Rais kutoa maelekezo ya kuchunguzwa," alisema.

"Baraza Kivuli la Mawaziri ninaloliongoza litaenda kuhakikisha Watanzania wanachagua mabadiliko ya kweli, yatakayowatoa kwenye uonyonge, uonevu na dhuluma," aliongeza.

Mchinjita alisema kwa mwaka huu, chama hicho kimeazimia kupigania mageuzi ya kidemokrasia, kupinga sheria kandamizi, kujenga taifa la wote, haki za ardhi kwa wananchi, huduma za matibabu kwa wote, hifadhi ya jamii kwa wananchi wote, haki za wafanyabiashara ndogo ndogo na bei nzuri ya mazao kwa wakulima.

Mchinjita ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Tanzania Bara, alikumbusha kuwa mwaka 2025 ni wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, hivyo kuwataka wafuasi na viongozi wa vyama vingine vya upinzani kuunganisha nguvu ili kuikabili CCM.

"ACT Wazalendo imedhamiria kujenga taifa la wote kwa maslahi ya wote. Si taifa la wachache wanaofaidi keki ya taifa gharama za wananchi wa kawaida, si taifa la watu wachache tu ndio wenye hakika ya matibabu, pensheni na viinua mgongo, si taifa la watu wachache ndio wenye haki ya kuishi kwa furaha. Sio taifa la viongozi ndio wanaoneemeka.

"ACT Wazalendo tunatoa wito kwa vyama makini vya upinzani, tukae pamoja na kujadiliana namna bora ya kuikabili CCM, tunahitaji umoja na mshikamano thabiti wa kuwahakikishia watanzania kuwa tuko tayari kuwapa matumaini," alisema Mchinjita.

Kuhusu gharama kubwa ya matibabu na kupendekeza kuwa serikali ije na mpango wa bima ya afya kwa wote.

"Huduma za afya zinapaswa kuwa haki inayopatikana kwa kila mtu bila kujali hali yake ya kifedha. ACT -Wazalendo tunaitaka serikali kuwekeza fedha ili kugharamia matibabu kwa watu wote nchini kwa kuwapatia Watanzania wote bima ya afya isiyo na matabaka," alisema.

Alisema gharama kubwa za matibabu zinaongeza ugumu wa maisha kwa wananchi wengi. Alipendekeza pia serikali iajiri walimu, madaktari, wauguzi na wataalamu wa kilimo, ili wananchi wapate huduma bora za kijamii za uhakika.

Kuhusu ubadhirifu wa fedha za umma, Mchinjita alisema chama hicho kinaitaka serikali iwachukulie hatua wahusika na kwamba hatua hiyo itadhibiti mianya ya wizi serikalini.

Aidha, kuhusu mikopo umiza, alisema ripoti zinaonesha kuwa wanaoumia ni wananchi wenye kipato cha chini na kuitaka serikali kutengeneza sera madhubuti ili kudhibiti utoaji mikopo kiholela.

"Kukosekana kwa mifumo salama ya mikopo kunawafanya wananchi kukosa fursa za kiuchumi, huku taasisi za kifedha zikiendelea kunufaika kwa kuwanyonya wananchi," alisema.

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024, alisema ACT-Wazalendo iliamini R4 za (Maridhiano, ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga Upya Taifa), zingetumika kuimarisha demokrasia, lakini imekuwa kinyume chake.

Alisema kutokana na kutoridhishwa na uchaguzi huo, tayari kimefungua kesi 51 katika maeneo mbalimbali nchini, kuupinga.

Kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, alisema chama hicho kitatumia mbinu zingine kumkabili mgombea wa CCM.

"Bila kufanya hivyo au kwa kudhani kwamba kuna maridhiano, tutaingia kwenye hadaa na kucheza mchezo mchafu ambao unaweza kuiharibu nchi yetu," alisema.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# BoT yapigilia msumari onyo matumizi ya fedha za kigeni

**Na Halfani Chusi**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imewaonya wanaotumia fedha za kigeni kufanya miamala nchini ikisisitiza kufanya hivyo ni kuhujumu uchumi wa nchi na ni kosa kisheria.

Pia imesema Kikao cha Kamati ya Sera ya Fedha kimeamua kuendelea na kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) cha asilimia sita katika robo ya kwanza ya mwaka 2025.

Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitoa taarifa ya kamati sera ya fedha kuhusu riba ya Benki Kuu kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka 2025.

Alisema mtu anapofanya miamala ya ndani ya nchi, anatakiwa kutumia saratu ya Tanzania na kusisitiza kuwa anayefanya kinyume, anahujumu uchumi wa nchi kwa sababu anatumia sarafu za nchi zingine.

Kuhusu kutokubadili riba, alisema, uamuzi huo unalenga kuhakikisha kiwango cha ukwasi kinaendelea kuwa cha kutosha katika uchumi, kudhibiti mfumuko wa bei kubaki chini ya lengo la asilimia tano na kuwezesha kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kufikia takriban asilimia 5.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2025.

Aliongeza uamuzi huo unalenga kuwa na utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni ili kuendelea kuwa na mfumuko wa bei ndogo utakaochangia jitihada za kuwafanya wananchi kutofanya miamala yao kwa kutumia fedha za kigeni nchini.

Kuhusu mwenendo wa uchumi wa dunia, alisema kamati ilibaini kuwa ripoti zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki ya Dunia, zinaonesha ukuaji wa uchumi unakadiriwa kuwa imara katika mwaka 2024.

Alisema katika robo ya nne ya mwaka 2024, kamati ilibaini mazingira ya uchumi duniani yaliimarika kwa kiwango kikubwa, kasi ya ukuaji wa uchumi ilongezeka, mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi, na mazingira ya upatikanaji wa fedha kwa riba nafuu katika masoko yaliimarika.

Mazingira mazuri ya kiuchumi, alisema yanatarajiwa kuendelea katika robo ya kwanza ya mwaka 2025 kutokana na ongezeko la mahitaji ya walaji, sera wezeshi za bajeti na kuimarika kwa mazingira ya upatikanaji fedha kwa riba nafuu huku akihadharisha kwamba yanaweza kuathiriwa na migogoro ya kisiasa duniani na mivutano ya kibiashara kuongezeka.

"Uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar umeendelea kuwa imara kwa mwaka 2024. Uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa asilimia 5.4 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.6 katika robo ya tatu na asilimia 5.7 katika robo ya nne ya mwaka 2024.

"Kwa kuzingatia mwenendo huo, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuwa sawia na matokeo ya ukuaji wa asilimia 5.4 kwa mwaka 2024. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na ongezeko la shughuli za kilimo, usafirishaji, ujenzi, na biashara," alisema Tutuba.

Kwa upande wa Zanzibar, alisema uchumi ulikua kwa asilimia 6.8 katika robo ya kwanza na asilimia 7.2 katika robo ya pili ya mwaka 2024 na ulikadiriwa kukua kwa viwango hivyo kwa robo mbili zinazofuata, hivyo kufikia matokeo ya ukuaji wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2024.

Alizitaja shughuli zilizochangia kukua kwake kuwa ni pamoja na utalii, ujenzi, na viwanda na kwamba katika mwaka huu, ukuaji wa uchumi kwa Tanzania Bara na Zanzibar unatarajiwa kuendelea kuwa wa kasi ya kuridhisha, kwa takriban asilimia sita na asilimia 6.8, mtawalia.

"Ukuaji huu unatarajiwa kuchangiwa na ongezeko la uzalishaji katika shughuli za kilimo, utekelezaji wa miradi ya ujenzi, maboresho katika usafirishaji na ugavi, nishati ya uhakika, pamoja na utekelezaji wa sera za fedha na kibajeti.

"Ukuaji wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa wa kasi ya kuridhisha mwaka 2024, ambapo ulifikia wastani wa asilimia 12.5 na asilimia 16.9, mtawalia," alifafanua Tutuba.

Alisema ukwasi wa fedha za kigeni uliongezeka kwa kiwango kikubwa katika robo ya nne ya mwaka 2024. Hali iliyotokana na kuimarika kwa mazingira ya upatikanaji fedha duniani kutokana na kupungua kwa riba katika nchi zinazoendelea na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni nchini kutokana na shughuli za utalii, mauzo ya dhahabu, korosho na tumbaku.

Pia alisema thamani ya shilingi inatarajiwa kuwa imara katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, kutokana na kuwapo kwa ukwasi wa kutosha wa fedha za kigeni uliopatikana katika robo ya nne ya mwaka 2024, utekelezaji wa sera ya fedha kutokana na uamuzi wa kubakiza Riba ya Benki Kuu kuwa asilimia sita na bei za bidhaa katika soko la dunia kuwa nafuu.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Washauri wazalishwe wataalamu, si wahitimu

**Na Maulid Mmbaga**

WAFANYABIASHARA wameshauri serikali kuwekeza katika kuzalisha wataalamu watakaolisaidia taifa kuelekea miaka 25 ijayo badala ya wahitimu ambao wengi hawakidhi vigezo katika soko la ajira.

Pia wameshauri kuwa katika nguzo za rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, kuanzishwe rasmi elimu rasmi ya biashara kuanzia shule za msingi, ili wanafunzi wawe na uelewa wa kutosha na kwamba mitaala ya elimu kuzingatia hilo.

Mfanyabiashara Benson Mahenya, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati wa mkutano wa Tume ya Mipango na wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda nchini, uliohusu kuhakiki rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

"Kuna uhaba mkubwa sana wa wataalamu nchini. Bahati mbaya nguvu kubwa imeelekezwa katika uzalishaji wa wahitimu ambao kwa kiasi kikubwa hawafiki kwenye soko la ajira. Nchi yetu bado inaingiza wataalamu kutoka nje kwa sababu haizalishi wa ndani kwa kiwango kinachostahili. Mifumo yetu ya elimu izalishe watu ambao ni wataalamu watakaosaidia taifa.

"Kuna haja ya kufundisha elimu ya biashara kuanzia chekechea hadi vyuoni ili kuhakikisha vijana wetu wanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masuala muhimu ya kibiashara. Hiyo itasaidia kuzalisha wataalamu wazuri watakaolisaidia taifa," alishauri Mahenya.

Pia alisisitiza kuwa katika rasimu ya Dira ya Maendeleo 2050, kuwe na kifungu maalumu kinachoonesha mabadiliko ya sheria ambazo ni za zamani na kuweka za kisasa zitakazoendana na mazingira ya ufanyaji biashara ya sasa.

Naye Mfanyabiashara Satbir Hanspaul alisema matumizi ya mifumo ya kidijiti na Akili Mnemba (AI) yameongezeka maradufu miongoni mwa kampuni, benki na wafanyabiashara hata ambao wako mbali na miji kitu ambacho hakikuwapo kwa miaka 25 iliyopita.

Alisema kwenye rasimu ya dira hawajaona jambo hilo likiangaliwa sana kwamba Watanzania tunatumiaje fursa ya AI, huku akishauri kuwa ni muhimu kukawa na kituo maalumu kitakachofundisha teknolojia hiyo, ikiwamo shuleni ili kuwafanya wanafunzi na Watanzania kwa ujumla kuwa na uelewa wa kutosha.

Pia alishauri kuwa ni muhimu Tanzania pia kujifunza mazuri yanayofanyika katika nchi zilizoendelea kwa kuwezesha Watanzania kuzitembelea nchi hizo kisha kuwarudisha kwa ajili ya kuliendeleza taifa.

"Sisi vijana wetu wengi wanatoka nje ya nchi, wakitoka hawarudi. Marafiki wenzangu shuleni tulikwenda nchi fulani, tulikuwa kama 20 lakini tulirudi wawili," alishauri Hanspaul.

Aidha, alipendekeza kuwa kwenye elimu, kuna umuhimu wa kuwa na mitaala yenye kujumuisha masomo ya uchumi na biashara kwa kiasi kikubwa kwa kuwa Watanzania wengi wamekuwa na tatizo la kushughulika na masuala ya fedha jambo ambalo alisema linalirudisha taifa nyuma.

Hussein Sufian, alisema iko haja ya kuboresha huduma zinazopatikana katika biashara binafsi kwa kuwa na miradi mikubwa ya kimkakati hasa katika uwezeshaji wa upatikanaji wa mikopo itakayotumika katika uzalishaji.

"Kuna upungufu mkubwa kwenye sekta ya kilimo, sehemu kubwa ya watu wanaofanya katika sekta hiyo hawana fursa ya kupata mikopo kwasababu watu hawana imani nayo ni changamoto kubwa. Wakulima wamesahauliwa licha ya kuwa kwenye mnyororo wa uongezaji thamani," alisema Sufian.

Naye Dk. Judith Mhina, alipendekeza kuwa serikali iweke dira ya maendeleo ya miaka 200 ijayo badala ya 25, akisema hiyo itasaidia kuwa na mfumo mzuri wa kutenga maeneo kwa kuzingatia ukubwa wa eneo la taifa ambayo yataonesha wapi pametengwa kwa ajili gani.




Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akimkabidhi zawadi Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa, alipomtembelea ofisini kwake Mtumba jijini Dodoma jana, kwa lengo la kumuaga baada ya kumaliza muda wake nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Utalii Tanzania kutangazwa miji 350 duniani

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) imeingia makubaliano na Shirika la Ndege la Uturuki kutangaza utalii wa Tanzania duniani kupitia safari za ndege za shirika hilo.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii na wawekezaji wa sekta hiyo nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TTB, Ephraim Mafuru, alisema jana kuwa wamechagua shirika hilo la ndege kwa sababu lina zaidi ya ndege 490 na linafanya safari zake katika zaidi ya miji 350 duniani na zaidi ya miji 60 kwa Afrika, hivyo Tanzania itatumia fursa hiyo kutangazwa vizuri katika miji hiyo yote duniani.

Alisema wameingia makubaliano na shirika hilo katika maeneo kadhaa ili kutoa matangazo ya vivutio vya utalii na maeneo ya uwekezaji katika ndege zao, kupitia tovuti na ofisi zao zote duniani na fursa ya punguzo la nauli kwa abiria hasa wa Tanzania kwa safari zenye lengo la kutangaza utalii wa Tanzania.

Mafuru pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuifungua nchi hasa katika sekta ya utalii duniani.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Ndege la Uturuki nchini Tanzania, Kadir Karaman, alisema makubaliano hayo yataimarisha lengo la pamoja la kuifungua Tanzania kwenye masoko ya utalii ya kimataifa, ukuaji na manufaa kwa pande zote.

# Madiwani waona fursa uwekezaji muundo PPP

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPPC), kimesema mwisho wa mwezi huu kitatuma wataalamu kwenda Manispaa ya Ilemela jijini Mwanza, kwa ajili ya kuangalia maeneo muhimu ya miradi ya ubia.

Uamuzi huo umekuja baada ya madiwani wa Manispaa ya Ilemela kutembelea PPPC jana kujifunza namna kinavyofanyakazi na watakavyotumia rasilimali ardhi waliyonayo kutekeleza miradi ya ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma.

Mkurugenzi Mkuu wa PPPC, David Kafulila aliyasema hayo jana wakati akizungumza na madiwani wa manispaa hiyo ambao pia miongoni mwao alikuwapo Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Angelina Mabula, Meya wa Ilemela, Renatus Mulunga na Mwenyekiti wa CCM, Yusuph Bujiku.

Alisema uamuzi wa manispaa hiyo ni mzuri kwa kuwa wataendesha miradi kwa kutumia mtaji wa umma ambao unapatika kwa ubia na sekta binafsi.

"Mmefanya uamuzi sahihi kuja kututembelea, mjifunze kwa kuona mradi wetu wa DDC ambao unatekelezwa kwa PPP ila tuna miradi mingine iliyopo katika hatua mbalimbali 82, na maeneo mengi ambayo mnaweza kuyaendeleza kwa mtaji wa umma," alisema.

Kafulila alisema ubia ni ndoa ya ushirikiano na si ubinafsishaji kama inavyoelezwa na kwamba miradi ya ubia yote ni mali ya serikali kabla, wakati na baada na sekta binafsi inaingiza mtaji na kuendeleza.

Aidha, alizitaja sababu za ubia kuwa ni kuvuna mtaji wa sekta binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya serikali badala ya kukopa na kwamba fedha ambayo serikali ingetumia kuwekeza itatekeleza miradi mingine maeneo ambayo sekta binafsi haijaona fursa.

Alizitaja sababu nyingine za uwekezaji kuwa ni kuvuta mitaji kutoka sekta binafsi, kuvuta teknolojia ambayo utafiti unaonesha ni sekta binafsi imepiga hatua eneo hilo.

Nyingine ni kuongeza ufanisi wa kiutendaji kwa kuwa sekta binafsi inamudu kusimamia mambo yake kwa ufanisi mkubwa bila urasimu kuliko ambavyo serikali ingefanya.

Nyingine ni uamuzi wa kiufanisi, huku akitoa mfano kuwa zipo sekta binafsi huajiri wakurugenzi wa mshahara mkubwa kwa kuwa wanachokitafuta ni ufanisi, kwa PPP sekta binafsi inaweza kununua mtaalamu mwenye ufanisi mkubwa kwenye utekelezaji wa miradi.

Kwa mujibu wa Kafulila, mahitaji ya binadamu yanaongezeka kila siku kuliko uwezo wa serikali yoyote duniani kuyamudu, na kwamba chanzo cha mapato cha serikali ni kodi na mikopo, haiwezi kumudu kuyatimiza bila PPP.

"Uzoefu unaonyesha kuwa serikali haiwezi kufikia matarajio kwasababu inategemea kodi na mikopo. Deni la dunia kwa sasa ni dola trilioni 300 huku uchumi ukiwa ni Dola trilioni 110 ambayo ni mara tatu ya uchumi," alisema.

"Huwezi kutimiza mahitaji kwa kukopa, lazima ualike sekta binafsi ije na mitaji yake itekeleze, kwa kutumia PPP unatekeleza miradi bila kugusa bajeti na kupunguza shinikizo kwenye vitabu vya serikali. Ilemela mmefanya uamuzi sahihi," alisema Kafulila.

Aidha, alisema michuano ya AFCON 2027 ni fursa kwa Tanzania kutumia PPP kujenga viwanja na huduma nyingine muhimu na kwamba ni muhimu ikaangaliwa kama fursa ya kiuchumi.

Naye Meya wa Manispaa ya Ilemela, Renatus Mulunga, alisema wapo tayari kwa kuwa wana maeneo mengi ambayo yanaweza kutumika kutekeleza miradi kwa ubia na ndio sababu ya kujifunza ili wafanye uamuzi sahihi anapopatikana mwekezaji.

Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Angelina Mabula, alisema Manispaa hiyo ilishatenga maeneo ila haijapata mwekezaji na kwamba wameona PPP ndio njia sahihi.

"Tuna eneo la Mahombolo tunaweza kujenga viwanja hasa kwa ajili ya AFCON, tunahitaji kituo cha mabasi na soko la kisasa, hii hatuwezi kutekeleza kwa bajeti za manispaa bali kwa PPP," alisema.

HABARI KITAIFA

# Jela miezi sita kwa kukutwa na sare za JWTZ

## ⬢ Ajitetea alifanya hivyo ili asikataliwe na mchumba

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

RAJABU Reli (22) amehukumiwa kifungo cha miezi sita gerezani baada ya kukutwa na hatia ya kuvaa na kutembea na sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kinyume cha sheria.

Shauri hilo la jinai namba 445/2025 lilitolewa hukumu juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza, Evodius Kisoka.

Awali akisoma hati ya mashtaka mbele ya Hakimu, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Nyamhanga Tissoro alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Desemba 5, 2024 katika kijiji cha Kasisa, wilaya ya Sengerema kinyume cha kifungu cha 178(1) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, SURA 16, marejeo ya mwaka 2022.

Mshtakiwa alifikishwa mahakamani huko Januari 7, 2025 na kusomewa shtaka la kuvaa sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania bila ruhusa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mshtakiwa huyo alikiri kosa na kueleza kuwa alifanya hivyo ili aweze kukubaliwa na mchumba wake na kuwa kosa hilo amelifanya mara moja tu.

Mahakama hiyo ilipokea ushahidi wa sare hizo alizokuwa akizivaa kisha kusikiliza pande zote za ushahidi ambako Hakimu Kisoka alijiridhisha kuwa ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri ni mzito na haukuacha shaka lolote.

Hakimu Kisoka alitoa nafasi kwa mshtakiwa huyo kujitetea kwanini asipewe adhabu kali. Naye akaomba mahakama hiyo imwachie huru kwa kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza.

"Mheshimiwa Hakimu, ninaomba nisamehewe kwa kuwa ni kosa la kwanza na nilivaa na kwenda kumwonesha mchumba wangu kuwa mimi ni askari ili asinikatae," alidai.

Hata hivyo, Hakimu Kisoka alitupilia mbali ombi hilo na kutoa hukumu hiyo ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama ya Rajabu.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga simu / sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Wakulima wa skimu ya umwagiliaji Tubugwe Juu wilayani Kongwa mkoani Dodoma wakiwa na wataalamu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), walipotembelea miundombinu ya umwagiliaji ya skimu hiyo ikiwa ni sehemu ya mafunzo ya Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula nchini (TFSRP - P4R). **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Upatikanaji dawa Muhimbili sasa wafikia asilimia 98

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imeongeza wigo wa upatikanaji wa dawa na kufikia asilimia 98 kutoka asilimia 70 ya awali.

Uongozi wa hospitali hiyo ulibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam mbele ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyozuru hospitalini huko kupata uzoefu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya ziara katika jengo la huduma ya dharura kwa watoto MNH, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo na Kanuni - Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mihayo Juma Nungu, alisema MNH ni kioo kwa nchi na Afrika Mashariki.

Alisema huduma zinazotolewa na MNH zimeboreka kulinganishwa na miaka 10 iliyopita, hivyo wameamua kuzuru hospitalini huko ili kupata uzoefu wa utoaji huduma, hususan namna ya kuwahudumia wagonjwa kwa kutumia bima ya afya.

"Zanzibar tuna mwaka mmoja wa kutoa huduma kwa bima ya afya na Tanzania Bara ni takribani miaka 25, hivyo uzoefu walio nao MNH huweza kulinganisha na pengine.

"Kwa sababu hospitali hii inahudumia kitaifa na si Tanzania tu bali hata nchi jirani. MNH ni kioo cha huduma za afya kwa nchi za Afrika Mashariki," alisema Nungu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Bima za Afya Zanzibar (ZHSF), Mbarouk Omar Mohammed, alisema kamati imetembelea hospitalini huko kwa kuwa huduma wanazotoa zinakwenda na wakati.

"Zanzibar tunaweza kujifunza kutoka MNH, kwa sababu hata huduma wanayotoa si ile ya zamani. Wanakwenda na wakati, tumekuja kuboresha ushirikiano na MNH," alisema Mohamed.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MNH na Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji MNH, Dk. Rachel Mhavile, alisema yapo mabadiliko kwenye hospitali hiyo hasa katika utoaji huduma kutokana na uwekezaji.

Alisema hospitali hiyo ya taifa imekuwa sehemu ya utoaji uzoefu kwa huduma za afya kutokana na kuwapo madaktari bobezi na bingwa, utoaji huduma za kibingwa na upatikanaji dawa kwa bei nafuu kulinganishwa na kwingineko.

"MNH tunajivunia utoaji huduma, majengo, vifaatiba vya kisiasa, dawa, mabingwa wazawa, miaka michache ijayo tutakuwa na Muhimbili mpya kutokana na ukarabati unaoendelea," alisema Dk. Mhavile.

Meneja wa Mkoa wa Ilala wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Dk. Aifena Mramba, alisema mfuko huo uko tayari kushirikiana na wenzao wa ZHSF, ili wafike lengo la utoaji huduma kwa njia ya bima.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA NJONBE, RUKWA, SONGWE NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA ZA NYASA, MBINGA, MJI WA MBINGA, WILAYA YA SONGEA NA MANISPAA YA SONGEA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na route ya tisa utafanyika katika Mikoa ya Njombe, Rukwa, songwe na Ruvuma katika Halmashauri ya Wilaya za Nyasa, Mbinga, Mji wa Mbinga, Wilaya ya Songea na Manispaa ya Songea tarehe 12 hadi 18 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumapili tarehe 12 hadi siku Jumamosi tarehe 18 Januari, 2025.
2. VITUO: Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika katika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa leo tarehe 03 Januari, 2024 na:

**Kailima, R. K**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218312902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upimaji maradhi ya moyo sehemu za kazi ni mwafaka, uungwe mkono

**MARADHI** yasiyo ya kuambukiza yamekuwa yakiongezeka nchini mwaka hadi mwaka, hivyo kusababisha nguvu kazi ya taifa kudhoofika na hata kupoteza maisha. Maradhi hayo ni pamoja na magonjwa ya moyo, figo, shinikizo la juu la damu na kusukari.

Kwa mujibu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), magonjwa hayo yamekuwa yakitumia mabilioni ya shilingi kwa ajili ya matibabu, hivyo kutishia ustawi wa mfuko huo.

Katika hospitali kubwa nchini, ikiwamo Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), kumekuwa na taarifa kwamba wagonjwa wengi wanakwenda kupata huduma ya tiba wakiwa katika hatua za mwisho. Hali hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa vifo vviitokanavyo na maradhi hayo. Licha ya vifo hivyo, pia wako watu ambao wamekuwa wakipata matatizo ya kuona na kukatwa baadhi ya viungo vyao kutokana na maradhi ya kisukari.

Sababu kubwa inayochangia ongezeko la maradhio hayo ni watu wengi kutokuwa na utamaduni wa kupima afya mara kwa mara. Watu wengi huenda hospitalini kwa ajili ya uchunguzi na tiba baada ya afya zao kudhoofu na kukosa nguvu za kuzalisha mali.

Chanzo kikubwa cha maradhi hayo ni mfumo wa maisha uliosababishwa na watu kula vyakula bila mpangilio hasa vile vya kusindikwa, kula wanga mwingi na nyama nyekundu kwa kiasi kikubwa na kutokufanya mazoezi.

Kwa wale wanaofanya kazi ofisini, wakiwamo walio katika nafasi za uongozi, wamekuwa wakikaa ofisini muda wote na wanapomaliza kazi huingia kwenye magari kurejea nyumbani. Wanapofika nyumbani wanakaa kuangalia runinga, kula kisha kulala, hivyo kuwa na uwezekano mkubwa wa kukumbwa na maradhi hayo.

Kutokana na kuwapo ongezeko la maradhi hayo, JKCI imeanzisha huduma ya kuwapima afya ya moyo wafanyakazi wanapokuwa ofisini ikiwa moja ya njia za kukabiliana na tatizo hilo. Uamuzi wa kuanzisha mpango huo umetokana na kubainika kuwa kuwa baadhi ya watu wanashindwa kwenda kupima afya zao kwa kutingwa na majukumu yao ya kila siku.

Taarifa iliyotolewa na kitengo cha masoko cha taasisi hiyo juzi ilisema imebainika kuwa wanafanya mazoezi bila kujua afya zao na wengine wanapata msongo wa mawazo wakiwa kazini, wengine wanaanguka na kupata matatizo mbalimbali kama kiharusi, hivyo mpango huo umeanzishwa kujaribu kunusuru tatizo hilo.


Iwapo watu watakaofikiwa na huduma hiyo watabainika kuwa na tatizo, taasisi hiyo imesema wataanzishiwa matibabu mapema kabla ya kuwa katika hali mbaya. Kama ilivyoeleza katika taarifa yake, programu hiyo itasaidia kupunguza gharama za matibabu kwa watu ambao wanagundua matatizo yao ya afya zao hali ikiwa mbaya kwa kuwa utambuzi wa tatizo katika hatua za awali hupunguza gharama za matibabu.

Kwa ujumla, mpango huo ni mwafaka na umebuniwa katika muda ambao huduma za matibabu zikiwamo upimaji wa afya zikiwa zinahitajika kwa kiwango kikubwa. Kwa mantiki hiyo, mpango huo unapaswa kuungwa mkono na wadau mbalimbali wakiwamo waajiri kwa kupanga muda maalumu kwa wafanyakazi wao kupatiwa huduma za upimaji.

Kwa kuwa mpango huo una lengo la kuhakikisha rasilimali watu nchini inakuwa na afya bora, wadau pia hawana budi kujitokeza kuunga mkono kupitia udhamini wa aina mbalimbali. Mpango huo una gharama kubwa zikiwamo usafiri na vifaa, hivyo taasisi zinaweza kutoa msaada kwa watumishi wa JKCI kuwafikia walengwa na kufanikisha jambo hilo kwa ufanisi mkubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Tuntule Swebe

## Muungwana Lazima Nilonge

# Januari ni ngumu kwa haya, tuipambanie kwa namna hii

**IMEZOELEKA** kipindi cha mwezi huu Januari, kuna mambo magumu kwenye familia nyingi na sababu inaangukia kwenye matumizi makubwa, yakiwamo ambayo yasiyo rafiki nyumbani.

Matokeo yake, huwafanya wengine kupitia changamoto mbalimbali, kwa sababu ya mpangilio usio mzuri wa bajeti zao.

Baadhi ya wazazi wanafafanua jinsi mwezi wa kwanza unavyokuwa mgumu kwao. Hapo nina maoni ya Joyce Ngowi, mkazi wa Kimara, jijini Dar-es Salaam, anayeufafanua mwezi Januari, ugumu wake unawagusa baadhi ya watu wanaosafiri, wakitumia pesa kwa ajili ya nauli na hata wanapofika huko, wanaangukia bajeti nyingine kama kusaidia ndugu.

Akiendelea, akasema na wengine hufanya sherehe, ikiwamo kwa baadhi katika staili ya mjumuiko fulani na hilo linashuhudiwa sana mkoani Kilimanjaro, ikiwa mithili ya mila.

Kila ifikapo mwisho wa mwaka, huambatana na mengi, ikiwamo katika imani; sherehe kama za komonio.

Upande mwingine, ni tarehe zinasuburiana na ulipaji kodi za wapangaji vyumba, wanajikuta wanakopa, alimaliza kwa kusema watu wanapofika mwezi wa Januari wanatumia kulipa madeni na ada za shule kwa watoto, hivyo majumuisho yake ni kunaangukia mzigo wa changamoto.

Wazazi waliendelea kutoa changamoto zao, mkazi wa Bondeni, Dar-es Salaam (jina ninalo), ana yake ya kuainisha mwezi husika na changamoto aliyo nayo binafsi.

**Wazazi waliendelea kutoa changamoto zao, mkazi wa Bondeni, Dar-es Salaam (jina ninalo), ana yake ya kuainisha mwezi husika na changamoto aliyo nayo binafsi.**

Anasimulia, mkewe kamwomba pesa za safari na zawadi kupeleka kwao kusalimia, lakini hilo limekuwa mzigo wa ziada kila anapotafakari shule zinafunguliwa, akiwa na uhitaji wa kumgharamia mwana anayesoma, anajikuta ana wakati mgumu.

Kama hilo, analo mzazi mwingine Pajrasi Hamadi, mkazi wa Goba, Dar es Salaam, akiutaja mwezi wa kwanza unakuwa mgumu kwake, kwa sababu ya bajeti za mwisho wa mwaka kuwa juu, wao wazazi wanakuwa na matumizi makubwa kipindi hicho.

Akaendelea kufafanua kwamba ni kipindi hata kwa kampuni nyingi, mauzo yake yanashuka, hivyo zinapata changamoto.

Mtazamo wa mzazi huyo ni kwamba, wao kada ya wazazi huangukia matumizi makubwa bila ya kuwa na akiba, zao lake wanaangukia kuyumba kiuchumi, ikiwamo katika mlo.

Mzazi mwingine, mkazi wa wilayani Kilombero, Morogoro asiyependa kutajwa jina gazetini, ana hoja ya kuwa ni kipindi cha kuanza kuandaa mashamba kwao wakulima, hivyo inawawia vigumu kumpatia mtoto mahitaji ya shule.

Akihitimisha kwa kuiomba serikali kuwawekea mkazo walimu, kuvumilia mapungufu ya watoto wakati huo.

Mzazi mwingine anayeishi Goba, Dar-es Salaam, mwenye mkazo mahususi katika ugumu wa kutatua ada za shule, pamoja na mahitaji yake kama vile sare, vifaa vya masomo, madaftari na begi la kiuanafunzi.

Mzazi huyo anajitambulisha kuwa na mtoto anayejiunga na kidato cha kwanza, mwingine yuko kidato cha tano, ada zao zote zinatakiwa mwezi huu.

Hilo analitaja kwamba limeendana na mengine ya kijamii, mwezi uliopita baadhi kawafanyia sherehe za kipaimara, zikiungana Krismasi, kwake mwenye kipato kidogo ikabaki mtihani mkubwa.

Ni bahati inabaki kuwa wajibu usiepukika, kuianzia ndani ya Sheria ya Mtoto na zinginezo zinazohusu ustawi wa jamii, ikiwamo Sheria ya Elimu.

Bila shaka ni vema wazazi wakajizatiti kwa vitu muhimu vya lazima kwa watoto wao kama vile elimu. Kibusara, kwa majukumu ya kijamii yaliyowazidi uzito wasigeuze nayo ya lazima, cha muhimu katika yote ni kupambania haki zao za msingi.

Tutakiane wote, Heri ya Mwaka Mpya, mapambano mema kwenye kuleta maendeleo!

**HABARI KITAIFA**

# Kesi inayowakabili wanandoa yaahirishwa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeshindwa kuendelea kusikiliza kesi ya tuhuma ya kujeruhi na kutoa lugha ya matusi zinazowakabili wanandoa Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54) kwa sababu hakimu anayeisikiliza yuko likizo.

Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania wenye asili ya India wanaoishi mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana, Dar es Salaam, wanakabiliwa na mashtaka manne wanayodaiwa kuyatenda Julai 21, 2023 kinyume cha sheria.

Kesi hiyo iliahirishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Beda Nyaki wa mahakama hiyo hadi Februari 13, 2025 kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Frank Rimoy na washtakiwa waliwakilishwa na Wakili Gabriel Mnyele. Wote walikubaliana na tarehe hiyo ilipangwa.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka manne waliyodaiwa kuyatenda Julai 21, 2023.

Katika shtaka la kwanza la kujeruhi linalomkabili Nathwan peke yake, anadaiwa kuwa Julai 21, 2023, akiwa eneo la Mrina-Kisutu ndani ya wilaya ya Ilala, Dar es Salaam kinyume cha sheria, alimsababishia madhara makubwa Kiran Kanabar kwa kuzamisha kichwa chake kwenye chokaa.

Katika shtaka la pili la shambulio la mwili linalomkabili Nathwan peke yake, inadaiwa kuwa katika tarehe hiyo na eneo hilo, alimsababishia madhara Kiran katika mwili wake kwa kumpiga ngumi na mateke kichwani.

**Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania wenye asili ya India wanaoishi mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana, Dar es Salaam, wanakabiliwa na mashtaka manne wanayodaiwa kuyatenda Julai 21, 2023 kinyume cha sheria.**



Bingwa wa Magonjwa, Tiba ya Dharura na Ajali, MNH, Juma Mfinanga (kulia), akitoa maelezo kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ilipofanya ziara hospitalini hapo ili kupata uzoefu jana, jijini Dar es Salaam. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Adaiwa kumuua mwanawe kisa kutorudisha chenji 9,000/-

**Na Mwandishi Wetu,**
SONGWE

Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe linamshikilia Festo Nzuki (39), mkazi wa kitongoji cha Izyila, kata ya Mlowo, wilayani Mbozi kwa tuhuma za mauaji ya mtoto wake.

Mtoto huyo alifariki dunia Januari 2 mwaka huu saa nne asubuhi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Songwe.

Ilidaiwa kuwa Desemba 30 mwaka jana, mtoto Jackson Nziku (10), mwanafuzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Ivwanga, alipigwa sehemu mbalimbali za mwili wake na mtuhumiwa ambaye ni baba yake mzazi kwa kutumia fimbo, mateke na ngumi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, SACP Augustino Senga, baada ya kuona mtoto amezidiwa ndipo Januari Mosi mwaka huu saa 01:15 usiku mtuhumiwa aliamua kumpeleka Hospitali ya Ilasi kwa ajili ya matibabu na baadaye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Songwe. Hata hivyo, mtoto huyo alifariki dunia wakati anapatiwa matibabu katika hospitali hiyo.

Kamanda Senga alisema jana kuwa uchunguzi wa awali unaonesha chanzo cha tukio hilo ni mtoto huyo kutorudisha chenji kiasi cha Sh. 9,000 aliyopewa na mtuhumiwa baada ya kuagizwa kununua chapati.

"Uchunguzi wa tukio hili bado unaendelea na pindi utakapokamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani," Kamanda Senga alisema.

Kamanda huyo pia alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe limethibitisha kutokea kwa ajali ya barabarani iliyohusisha guta MC 342 CVK aina ya TVS lililoacha njia na kupinduka na kusababisha kifo cha mtu mmoja.

Ajali hiyo ilitokea Januari 6 mwaka huu saa saba mchana mtaa wa Mwakakati, wilaya ya Momba ambapo Dereva Erasto Nzowa, mkazi wa Melerani aliendesha guta hilo likiwa limebeba mzigo mzito wa vifaa vya ujenzi. Alipokuwa akipita katika barabara ambayo inaendelea kujengwa huku ikiwa imemwagwa vifusi ambayo havikusambazwa ndipo guta hilo lilimshinda na kupinduka na mizigo hiyo kumfunika na kusababisha kifo chake.

"Mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi wa kitabibu katika Kituo cha Afya Tunduma na umekabidhiwa kwa ndugu zake kwa ajili ya mazishi.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe linapenda kutoa wito kwa wazazi na walezi kutowaadhibu watoto kupita kiasi, kwani huu ni ukatili na ni kinyume cha haki za watoto na binadamu.

"Pia linawataka madereva na watumiaji wote wa vyombo vya moto kufuata sheria za usalama barabarani bila shuruti. Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe halitasita kuchukua hatua kali dhidi ya mtu yoyote anayefanya vitendo vya ukatili kwa watoto, uvunjaji sheria za usalama barabarani na makosa mengine ya jinai," alionya Kamanda Senga.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED





Mafundi wakiendelea na ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kujazia Gesi Asilia (CNG Mother Station) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)




Madereva bajaji na magari wakiwa katika foleni ya kujaza gesi katika kituo kipya cha Tembo Energies Limited kilichoko Mount Meru, Tabata, jijini Dar es Salaam.

# Vituo vipya vya kujazia gesi magari, bajaji vyajengwa

**Na Halfani Chusi**

BAADA ya kuwapo malalamiko ya muda mrefu dhidi ya uhaba wa vituo vya kujazia gesi katika magari na bajaji nchini, hatimaye kilio hicho kimesikika, vituo vitatu vipya vikijengwa mkoani Dar es Salaam.

Mnamo Oktoba 3 mwaka jana, Nipashe ilichapisha ripoti maalumu ikiangazia madhila wanayopitia watumiaji wa vyombo vya moto vinavyotumia gesi, baadhi wakilazimika kukaa kwenye foleni kwa saa sita hadi nane kupata huduma hiyo katika vituo vitatu vilivyokuwapo Dar es Salaam kipindi hicho.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, baada ya kukagua juzi ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kujazia Gesi Asilia (CNG) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambao umefikia asilimia 80, alisema kuwa mwishoni mwa mwezi huu kituo hicho kitaanza kutumika.

Akiwa kituoni huko, Mataragio alisema kuwa awali serikali iliahidi kukamilika kwa mradi huo mwezi Desemba mwaka jana, lakini umechelewa kutokana na meli iliyokuwa imebeba mitambo hiyo kutoka China, kuchelewa kufika nchini.

> **"Pia kitakuwa na pampu nne za kujazia gesi zitakazoweza kuhudumia zaidi ya magari manane kwa pamoja," Katto alifafanua.**

"Mitambo imeshasimikwa, kinachoendelea kwa sasa ni kazi ndogondogo za kuunganisha mfumo wa umeme ili kituo kianze kufanya kazi.

"Ujenzi huo hadi kukamilika kwake utagharimu Sh. bilioni 14.5, ukijumuisha ununuzi wa magari tisa na ujenzi wa vituo viwili vya kujazia gesi kwenye magari katika maeneo ya Muhimbili mkoani Dar es Salaam na Kibaha mkoani Pwani," alisema Mataragio.

Meneja Msimamizi wa Mradi wa Gesi Asilia (CNG) kutoka Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (TPDC), Aristides Katto alisema kituo hicho kikikamilika kitakuwa kituo mama kitakachowezesha vituo vingine kwenda kuchukua gesi na kupelekea sehemu nyingine.

Alisema kituo hicho pia kitasaidia kwenye miradi ya gesi majumbani, viwandani na katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

"Kituo hiki kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kushindilia gesi zaidi ya magari 1,000 kwa siku na kitakuwa na uwezo wa kushindilia gesi kwenye magari matatu yanayochukua gesi na kuipeleka katika maeneo mengine.

"Pia kitakuwa na pampu nne za kujazia gesi zitakazoweza kuhudumia zaidi ya magari manane kwa pamoja," Katto alifafanua.

Katika ufuatiliaji wake, mwandishi amebaini kuwa mbali na kituo mama hicho kinachojengwa UDSM, vituo vingine viwili vipya vya kujazia gesi vinajengwa hivi sasa Dar es Salaam; kimoja kiko Mawasiliano, Manispaa ya Ubungo na kingine kiko Mount Meru, Tabata, ambacho tayari kimeanza kutoa huduma.

Kabla ya ujenzi wa vituo hivyo vipya, Dar es Salaam ilikuwa na vituo vitatu vya kujazia gesi kwenye magari. Viwili viko katika Jiji la Ilala maeneo ya Tazara na Uwanja wa Ndege na kimoja kiko Ubungo Maziwa katika Manispaa ya Ubungo.

# Mtandao wapunguza msongamano magerezani

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JESHI la Magereza nchini limesema Mfumo wa Ofisi Mtandao kusikiliza kesi za wafungwa na mahabusu umepunguza msongamano katika magereza mbalimbali nchini na kurahisisha utendaji kazi.

Hayo yalisemwa na Kamishna Jenerali Jeremiah Katungu wakati akizungumza na maofisa na askari wa jeshi hilo katika Baraza la Wafanyakazi lililofanyika Msalato mkoani hapa.

Katungu, alisema matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yanasaidia kufanya kazi nyingi kwa muda mchache tofauti na kutumia kalamu kuandika kwenye karatasi.

Alisema jeshi hilo limeanza kusikiliza kesi za mahabusu kwa njia ya mtandao na kupunguza msongamano wa mahabusu magereza mbalimbali nchini.

Alisema wameanza kutumia nishati safi ya kupikia katika magereza hayo ili kukabiliana na uchafuzi wa mazingira.

Aidha, uamuzi wa kutumia nishati safi ya kupikia magereza ni moja ya mafanikio makubwa iliyopata jeshi hilo kwa mwaka jana.

"Haya ni mafanikio makubwa sana tumeyapata katika mwaka 2024, tunaendelea kuboresha ili kuhakikisha nishati safi ya kupikia inatumika katika magereza mbalimbali hapa nchini," alisema.


Katungu aliishukuru serikali kwa uwekezaji ndani ya jeshi hilo na kuboresha utendaji wake.

Akielezea tathmini ya jeshi hilo kwa mwaka jana, alisema mafanikio waliyopata ni pamoja na kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu gerezani kwa kushirikiana na Mahakama, Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na wadau wengine.

Alihimiza ushirikiano, umoja na upendo miongoni mwa maofisa na askari huku akiwakumbusha kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura na kupata fursa ya kuchagua viongozi katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Awali, Kamishna wa Sheria na Uendeshaji wa Magereza, Nicodemus Tenga, alimshukuru Katungu kwa kuandaa baraza hilo ili kutoa tathmini ya utendaji wa jeshi kwa mwaka jana.

Tenga, aliwataka watendaji wote wa jeshi hilo kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.





# Mwigulu Nchemba awaagiza TRA kukusanya kodi bila huruma

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Fedha, Mwigulu Nchemba, ameagiza Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) kukusanya mapato bila huruma kwa wakwepaji kodi kwa kuwa wanarudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Nchemba alitoa agizo hilo jijini hapa juzi wakati akifungua kikao kazi cha siku tano cha wakuu wa mamlaka hiyo.

"Wakwepa kodi wanarudisha nyuma maendeleo ya nchi kwa hili nendeni mkashughulike nao bila uoga kwa kuwa sheria zinawalinda na taifa liko nyuma yenu," alisema.

Alisema kukwepa kulipa kodi kunasababisha kutengeneza taifa lisilo na usawa, hivyo maofisa wa mamlaka hiyo wanatakiwa kuacha woga kwa kuwa sheria inawalinda na nyuma yao hakuna mkubwa wala maarufu katika kukwepa kodi.

"Mambo yanayohusu ukwepaji wa kodi hayakubaliki na tusiogope lawama kwa kuwa maendeleo yanapatikana kupitia kodi hizo zinazokusanywa na serikali," aliongeza.

Pamoja na mambo mengine, Nchemba, aliitaka TRA kutafuta njia ya kushughulika na wafanyabiashara wadaiwa sugu badala ya kuangaika na biashara zao.

"Kufunga biashara au kukamata akaunti ya mfanyabiashara ya benki kuna sababisha watu kuacha kutumia mifumo ya kibenki na itakuwa vigumu kukusanya kodi, tutafute njia za kushughulika nao badala ya biashara zao," alisema.

Vilevile, aliitaka TRA kushughulika na stakabadhi za bandia za kielektroniki za EFD kudhibiti upotevu wa mapato ya serikali.

Nchemba, alisema hakuna uadui kati ya mlipakodi na mkusanya kodi bali kuwepo kwa uhusiano mzuri ili kutengeneza walipakodi wengi.

"Walipakodi sio watumwa bali kinachotakiwa ni kila mmoja kutimiza wajibu wake," alisema.

Kamishna TRA, Yusuf Mwenda, alisema katika kipindi cha miezi sita ya Julai hadi Desemba 31, mwaka jana mamlaka hiyo imevuka malengo ya ukusanyaji kodi kwa asilimia 104.

Kwa mujibu wa Mwenda, kiwango kinatokana na kila mwezi kukusanya zaidi ya kiasi mamlaka hiyo ilichopangiwa bila kutumia nguvu kwa kushirikiana na wafanyabiashara waadilifu.

Alisema Kampuni ya Uwekezaji ya DP Word katika Bandari ya Dar es Salaam, imechangia kuongezeka kwa makusanyo ya kodi mara dufu, shughuli za uchumi, uagizaji pamoja na usafirishaji mizigo

Hata hivyo, alisema ukwepaji kodi bado upo nchini na duniani na kwamba kupambana na genge la wanaojihusisha na vitendo hivyo ni shughuli ngumu.

Mwenda, alisema wataendelea kutoa elimu ya ulipaji kodi kwa hiari kupitia makundi ya jamii wakiwemo watu maarufu, wanasiasa, wasanii, vyombo vya habari na viongozi wa dini .



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, akicheza ngoma wakati akiwa ziarani Kata ya Galapo wilayani Babati, mkoani Manyara juzi. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Vitongoji vyasotea maji ya bomba miaka 63

**Na Godfrey Mushi,** SAME

HATIMAYE wakazi wa vitongoji vya Mahuu na Kavambughu vya Kata ya Same, mkoani Kilimanjaro, wameanza kupata maji ya bomba baada ya kukosa kwa miaka 63.

Juzi, Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni, alizuru vitongoji hivyo kushuhudia kwa mara ya kwanza maji yakitoka katika vilula vilivyojengwa na serikali kurahisisha upatikanaji wa maji ya bomba kwa wananchi.

Kasilda, alisema wakazi wa vitongoji hivyo, wamehangaika kwa muda mrefu kwa kukosa maji.

Mradi huo unatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Kiarabu, inayosimamia Maendeleo ya Nchi za Afrika (BADEA), Mfuko wa Ofd unaojumuisha nchi zinazozalisha mafuta (OPEC), Mfuko wa Maendeleo wa Kimataifa wa Saud na Mfuko wa Misaada wa Kuwait.

Akisoma taarifa ya mradi wa maji wa Mahuu na Kavambughu, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Same/Mwanga (SAMWASA), Rashidi Mwinjuma, alisema serikali imedhamiria kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wapatao 35,220 wa Same.

Mwinjuma, alisema serikali imetekeleza mradi wa maji awamu ya kwanza kwa kutoa Bwawa la Nyumba ya Mungu na kusambaza miji ya Mwanga na Same na vijiji vyote vilivyopitiwa na mradi huo.

Alisema kukamilika kwa mradi huo, kumewezesha miji hiyo kupata maji ya uhakika kwa vipindi vyote.

Alisema kwa sasa wanaendelea na kazi ya kuendeleza mitandao ya maji ili kuwasogezea wananchi huduma karibu.

"Wananchi hawa walikuwa wanalazimika kutembea umbali mrefu wa kilomita nane kufuata huduma ya maji, walikuwa wakinunua ndoo ya maji shilingi 300 mpaka 500, kukamilika kwa mradi kutaondoa adha hiyo," alisema Mwinjuma.

Alisema SAMWASA, walisanifu mradi wenye thamani ya zaidi ya milioni 40.8 kuwasaidia vitongoji vya Mahuu na Kavambughu vyenye wakazi 5,600.

Alisema mamlaka hiyo inaendelea kutekeleza miradi zaidi ya minane ndani ya Same, yenye thamani ya Sh. milioni 219.179 ili kuunganishiwa huduma katika kaya za wakazi wa mji huo.

Mradi huo mkubwa wa maji, umelenga kuwanufaisha zaidi ya wananchi 438,000.

## Polisi yaanza ukaguzi mabasi ya wanafunzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani hapa limeanza operesheni maalum kukagua mabasi ya shule yanayobeba wanafunzi kabla ya shule kufunguliwa mwanzoni mwa wiki ijayo.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani hapa, Zauda Mohamed, alisema lengo la ukaguzi huo ni kuondokana na ajali zinazosababishwa na ubovu wa mabasi ya shule.

Zauda, alisema ukaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa sheria za usalama barabarani kifungu cha 39 sura namba 68 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2002.

Aliwataka wamiliki wa shule na madereva kutoa ushirikiano kwa kuwa umebaki muda mchache shule kufunguliwa kwa kupeleka mabasi yao Kituo cha Polisi kukaguliwa.

Alionya kuwa jeshi hilo litaanza msako dhidi ya mabasi ambayo wamiliki wake wamekaidi wito huo wa polisi siku hiyo ya Januari 13, mwaka huu,


Wakizungumzia ukaguzi huo, baadhi ya wazazi, walezi wa wanafunzi wanaotumia mabasi hayo kwenda na kurudi nyumbani walipongeza jeshi hilo kwa hatua hiyo wakisema itawahakikishia usalama wa watoto wao wanaposafiri kwa mabasi hayo kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Gloria Lazaro, alisema baadhi ya masi hayo ni mabovu hali inayosababisha wazazi na walezi kuwa hofu juu ya usalama wa watoto wao wanapokuwa kwenye vyombo hivyo.

"Tuna imani ukaguzi huu utakuwa mwarobaini wa baadhi ya shule kutumia magari mabovu," alisema.

Kalanga Mollel, Mkazi wa Kwa Mrombo, alisema hatua hiyo ni nzuri na kutoa rai kwa jeshi hilo kuchukua hatua dhidi ya madereva wanaojaza wanafunzi kupita kiasi.

"Wazazi na walezi tunalipa nauli za watoto wetu kila shule zinapofunguliwa, lakini kuna wamiliki wanajaza wanafunzi kwenye mabasi hayo kupita kiasi na wakati mwingine wanapakatana," alisema.





# Wananchi 'wambebesha' mbunge wao kero lukuki

**Na Judith Julius,** NGARA

WAKAZI wa Kata ya Muganza, wamemtaka Mbunge wa Ngara, George Ruhoro, kutatua kero zinazowakabili tangu Tanzania ipate uhuru.

Wakazi hao walitaja moja ya kero hiyo sugu kuwa ni kata yao kukosa zahanati na kusababisha vifo vya wajawazito wakati wa kujifungua na watoto wachanga kutokana na matatizo mbalimbali.

Wakazi hao, walimtaka Mbunge Ruhoro kuhakikisha wanapata zahanati ili kudhibiti vifo vya wajawazito na watoto wachanga.

Wakazi hao, akiwamo January Raphael, walitoa kilio chao juzi wakati wa ziara ya Mbunge huyo kusikiliza kero za wananchi.

Raphael, alisema tatizo la ukosefu wa zahanati katika kata hiyo ni kubwa hali inayosababisha wajawazito kukosa huduma haraka wakati wa kujifungua na kusababisha baadhi yao kufa.

Mkazi mwingine, Elizabeth Thomas, alisema kata hiyo ina matatizo lukuki kwa kukosa huduma muhimu kwa mahitaji yao.

Elizabeth alitaja matatizo hayo kuwa ni pamoja na ukosefu wa Kituo cha Afya, ofisi ya walimu wa Shule ya Msingi Muganza, upungufu wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Msazo na ukosefu wa majisafi na salama.

Alisema kero hizo zimewatesa kwa muda mrefu hivyo kumuomba mbunge huyo kuhakikisha zinapatiwa ufumbuzi haraka iwezekanavyo.

Diwani wa Kata hiyo, Leonard Burindoli, alithibitisha kuwepo kero hizo na kuwasilisha mara kwa mara katika Baraza la Madiwani bila mafanikio.

Akipokea kero hizo, Mbunge Ruhoro, aliwataka wakazi hao kuendelea kuwa wavumilivu na kuahidi kuwasilisha bungeni hivi karibuni zipatiwe ufumbuzi kwenye bajeti ya mwaka wa fedha ujao wa fedha wa 2025/26.

Sera ya Afya ya mwaka 2007, kifungu namba 5(4) kutaka kila Kijiji kiwe na zahanati na kata kituo cha afya ili kuleta uwiano katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Hali hiyo ni tofauti kwa kata hiyo ambako kwa zaidi ya miaka 60 ya uhuru hawajawahi kupata hata zahanati.



Walimu wa somo la Fizikia, akiwamo John Samwel (kulia) kutoka Shule ya Sekondari Imalaseko mkoani Simiyu, na Yohana Maduhu (kushoto), Sekondari ya Bukundi, wakionesha jaribio la uhamishaji wa joto kwa njia ya mzunguko unaotumia kimiminika (liquid) na gesi, jana wakati wa mafunzo kwa walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Wilaya ya Tarime mkoani Mara. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RC, COPRA kuwainua wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Kenani Kihongosi, ameahidi kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) kuhakikisha mifumo ya serikali ya biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko inafuatwa na kumnufanisha mkulima na mfanyabiashara nchini.

Kihongosi alitoa ahadi hiyo jana ofisini kwake wakati akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa COPRA, Irene Mlola ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kuitambulisha mamlaka hiyo kwa watumishi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Alisema kama mkoa, watakuwa mstari wa mbele kuhakikisha ushirikiano baina yao na mamlaka hiyo unaimarika ili kutoa matokeo chanya kwa wakulima na wafanyabiashara hao.

"Tumefurahi ujio wenu hapa Simiyu, na imani mifumo ya biashara ya nafaka mchanganyiko itafuatwa kadri ilivyoelekezwa na serikali ili kunufaisha sekta ya kilimo," alisema Kiongosi.

Alisema anaamini wakulima na wafanyabiashara wa mazao hayo mkoani hapa watanufaika na mifumo hiyo, hivyo kama serikali wataendelea kutoa ushirikiano kuhakikisha kila mmoja anafaidika na fursa hiyo.

Kwa upande wake, Irene, alisema COPRA itafanya kazi kwa kushirikiana na viongozi wote kuanzia ngazi ya vijiji hadi mkoa ili kuhakikisha masoko ya nafaka na mazao hayo yanafanyika kwa kufuata miongozo iliyowekwa na serikali.

Alisema pia watahakikisha uuzaji mazao hayo kwa mfumo wa stakabadhi ghalani na kwa njia ya minada ya kidigitali hususani ya dengu, choroko, mbaazi, karanga, ufuta, iliki, karafuu, pilipili manga, kakao, soya na mdalasini utafanyika kwa kadri ilivyopangwa.

"Tunakushukuru mkuu wa mkoa kwa ushirikiano mnaotuonyesha, naamini tutaendelea kufanya kazi pamoja ili kuhakikisha tunafikia malengo tuliojiwekea," alisema Irene.

Alisema serikali imeweka taratibu rasmi za biashara hizo kwa lengo la kuwainua wakulima ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiuza mazao yao kwa bei ya chini ikilinganishwa na gharama kubwa za uzalishaji walizotumia.

Alisema kutokana na hali hiyo, wamekuwa wakiathiriwa kwa kutotumika kwa vipimo rasmi vilivyothibitishwa na kutambulika na mamlaka za serikali katika uuzaji wa nafaka na mazao hayo.

Hata hivyo, alisema COPRA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Serikali ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) itahakikisha wakulima wanapatiwa maarifa ya uzalishaji wa mazao bora kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema mamlaka huyo imepanga mikakati ya kuwainua kiuchumi wakulima na wafanyabiashara hao kupitia mifumo ya biashara na nafaka mchanganyiko.

# Wakerwa maji kutuama mitaroni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI ya Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga imeombwa kusimamia ujenzi wa mitaro katika barabara zilizopo Kata ya Majengo ili kudhibiti kutokea mlipuko wa magonjwa kutokana na maji kutuama.

Ombi hilo limetolewa na wakazi wa kata hiyo wakati wakilalamikia kutuama kwa maji hayo kwenye mitaro hiyo na mengine kutiririka kwenye makazi yao, hivi kuhatarisha maisha yao hususani watoto.

Mkazi wa Majengo, Benadetha Damas alisema, alishauri kuruhusu mitaro hiyo kupitisha maji na kudhibiti kuingia kwenye makazi yao na kuongeza kasi ya ujenzi ili ikamilike kwa wakati na kuondoa adha hiyo.

Aliipongeza serikali kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha mawasiliano na mkandarasi huyo kutoa kipaumbele cha ajira zisihitaji ujuzi kwa vijana wao.

Asteria Julius, alisema hivi karibuni shule zinatarajia kufunguliwa na isipotatuliwa adha hiyo baadhi ya wanafunzi watashindwa kupita.

Akijibu kero hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita mkandarasi amepewa taarifa na kwamba anashughulikia kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA).

Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Kahama, Masola Juma, alisema wanaendelea kufanya tathmini ya uharibifu wa barabara zote uliosababishwa na mvua na kuziboresha ili kurudisha mawasiliano kwa wananchi.

Juma, alisema pamoja na mvua kusababisha kupunguza kasi ya utekelezaji wa mradi huo, utakamilika kwa wakati kulingana na makubaliano ya mkataba.

Ujenzi wa barabara hiyo na mitaro hiyo, utagharimu Sh.bilioni 20.

ama
ALHAMISI JANUARI 9, 2025
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**KILICHOSHINDIKANA MIAKA, GHAFLA KIMEWEZEKANA... Kutana na mradi unaotatua migogoro mipaka, misitu vijijini Handeni, Kilindi**



**MSOMI WA KIAFRIKA... Mwanafunzi wa PhD anayebuni tiba ya kisukari kwa kutumia mwanga**

Ukurasa 12

# Safari ya Dk. Samia kusambaza huduma dharura hospitali inayookoa nusu ya vifo

## • Jina moja, jozi mambo matatu yananusuriwa...




Jengo mojawapo la huduma ya dharura hospitalini, katika hatua za uzinduzi.

**Na Mwandishi Wetu**

INAPOTANGAZWA dhana inayohusiana na huduma ya dharura hospitalini, hapo inagusa sura kuu kadhaa, kuwahisha kunusuru uhai wa mgonjwa aliye taabani.

Hiyo yaweza kuanzia anavyofikishwa kwa matibabu, anahudumiwa na safu ya wataalamu na watumishi tib ana nyenzo zinazotumika. Ni mara zote sura ya tiba kwa mgonjwa hunaziona anapoingia mikononi mwa matabibu.

Iwe ni kwa ajali au sababu nyinginezo kama ujauzito, mgonjwa huanza kuona sura ya ahueni safari yake kwenda kituo tiba inaanza, anapofikishwa katika mlango qwa kituo tiba, mikononi mwa wataalamu wanatumia aina nyenzo, iwe miundombinu kama vitanda na vile vya maabara.

Katika hilo, ndio Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameamua kulishikia kibwebwe kama sehemu ya mipango yake kuimarisha huduma ya afya kitaifa.

Zamani, msamiati "majengo ya kutoa huduma za dharura' au (EMD) kuwapo sana, sasa ni sehemu ya hospitali nchini, Wizara ya Afya ikiwa na ufafanuzi katika taarifa yake kipindi kama hiko mwaka jana kwamba:

"Miaka mitatu ya Rais Samia imewezesha kuanzishwa kwa majengo mahusus ya huduma za dharura na ajali (EMDs) 105 kutoka EMD saba zilizokuwapo mwaka 2020.'

Ufafanuzi wa Wizara ya Afya, unagusa maeneo ya hospitali maalum kama ya (Jakaya Kikwete - JKCI, Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili - MOI za Dar es Salaam; pia Benjamin Mkapa, Dodoma), za kanda kama Mbeya na mikoa kama vile; Kigoma na Lindi, pia wilaya kama Handeni.

"Kukamilika kwa ujenzi wa EMD kutapunguza vifo na kuokoa maisha kwa wagonjwa wa dharura na wa ajali kwa asilimia kati ya 40-50 kwa mujibu wa tafiti za kitaalam." Inafafanua Wizara ya Afya.

**MAGARI YA WAGONJWA**

Ni hatua inayoendana na kipindi hicho nchini kuingiza magari ya wagonjwa 727 mwaka mmoja uliopita, ikilenga kurahisisha utoaji wa huduma za matibabu ya dharura kwa wagonjwa wahitaji katika hali mbaya.

"Yamepelekwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini..." anatamka taarifa hiyo yenye ufafanuzi:

"Zinakwenda kusaidia kusafirisha wagonjwa, wakiwamo kinamama wenye changamoto za uzazi kwa haraka na kuwafikisha katika huduma za rufani, hivyo kupunguza adha kwa wananchi na kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika."




Huduma ya dharura katika Hospitali ya Mkoa Dodoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**RASILIMALIWATU TATIZO**

Katika mtazamo huo wa huduma dharura -EMD, mafanikio yake hukamilishwa na jitihada za wataalamu wanaowajibika mahali hapo pa afya.

Hapo ikumbukwe kuwa katika tafsiri ya utendaji tiba duniani, inaegemea kinachoitwa 'Labour Oriented Capital', nguvukazi inategemewa zaidi, kuliko mitambo, tofuti na 'Capital Oriented'; kunakotegemewa zaidi mitambo, kuliko rasilimaliwatu.

Hivyo, kuwapo safu inayotosha kwa idadi na stadi za kiutendaji, ina maana kubwa kwa ufanisi wa tiba ya mgonjwa na mahsusi huduma hiyo ya dharura.

Mgonjwa wa dharura anayochukuliwa na gari, huanza kupata huduma tiba pindi angiapo katika gari husika, ambako kunakuwapo wataalamu na huduma za dharura kumhudumia, akiwa safarini kwenda hospitalini.

Hilo ni eneo moja linalomsukuma Rais Dk. Samia katika zama za uongozi wake, kuajiri wataalamu kusaidia dharua na huduma nyingine, kupitia kauli za Wizara ya Afya mwaka jana:

"Jumla ya wataalamu 35,450 wa kada mbalimbali wameajiriwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2023. Aidha, jumla ya ajira za mikataba kwa watumishi wa Afya 2,836 kupitia miradi mbalimbali ya serikali zilitolewa...'

Wizara ya Afya inafafanua kutumia shilingi bilioni 22 hadi

Inaendelea Uk. 12

AFYA

## MSOMI WA KIAFRIKA...

# Mwanafunzi wa PhD anayebuni tiba ya kisukari kwa kutumia mwanga

**Na Mwandishi Wetu**

NI mwezi mmoja uliopita, Taasisi ya L'Oréal kwa pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), zilitangaza washindi wa Tuzo za Vijana wa Talanta kwa Wanawake katika Sayansi barani Afrika.

Hapo ikawatunuku kwa mwaka jana, watafiti 30 kutoka Afrika katika nyanja ya sayansi. Hao ni wanafunzi 25 wa shahada ya uzamivu (PhD) na wanafunzi watano wa ngazi, baada ya shahada ya uzamivu kutoka nchi 15 za Afrika.

Hapo ndipo anapopatikana mwanafunzi wa shahada ya uzamivu, kutoka nchini Benin, Marie Marthe Chabi, akipaishwa na utafiti wake katika sekta ya afya, akilenga ugonjwa unaozidi kuathiri Waafrika; kisukari.

Makadirio ya Shirika la Afya Duniani (WHO), ni kuwapo watu milioni 24 wanaotaabika na kisukari barani Afrika hadi kufika mwaka 2021, matarajio yaliyoko ni ongezeko la kufika milioni 55 ifikapo mwaka 2045; ziada ya asilimia 129.

Ugonjwa huo hadi sasa, unachukuliwa kuwa janga barani Afrika, unajitokeza kwa aina mbalimbali, kwa mujibu wa WHO.

Mwanafunzi wa shahada ya uzamivu katika sayansi ya biolojia, Marie Marthe Chabi, alichagua kutafiti kisukari cha aina ya pili, akiwa na sababu:

"Najua watu wanaosumbuliwa na ugonjwa huu na lazima kutambua kuwa wengi wao wana maisha ya 'uchochole' (ubabaishaji) kutokana na magonjwa yanayotokana na kisukari cha aina ya pili," anasema Marie. Mtafiti huyo anafafanua kwamba, kisukari kinatambuliwa kwa kiwango cha juu cha sukari kwenye damu na hali hiyo inapozidi, anaeleza kwamba: "Unatanuka hadi kuwa magonjwa kama ya moyo, magonjwa ya neva na hata matatizo ya macho."

Mtazamo wake kitaaluma anafafanua kuwa, kadri yanayohitajika kufuatiliwa ili kuwa na maisha bora yanavyopuuzwa, ndivyo ugonjwa unavyoendelea kuathiri na hata kusababishia vifo Waafrika wengi.

Marie anaendelea: "Ndio maana napigania kupambana na ugonjwa huu wa kisukari."

**TIBA YA MWANGA**

Ni tiba inayohusisha kutumia mwanga kwenye mwili wa mgonjwa, ili kugundua mifumo na njia za ishara zinazozuia au kupunguza ufyonzaji wa glukosi.



Mtafiti, Marie Marthe Chabi. **PICHA: MTANDAO**

Unatajwa kuwa mchakato mgumu zaidi, akiongeza kuwa anazingatia anachokitaja kuwa "mwanga mwekundu, mwanga wa sumaku umeme."

"Kweli mwanga ni nishati. Ni kama jua linalotupatia joto tunapokuwa baridi. Huu mwanga una chembe ndogo zinazojulikana kama 'photon' ambazo hutumika kama vyanzo vya nishati kwa mitambo midogo ya nishati inayopatikana mwilini iitwayo mitochondria."

Mtu anapomulikwa na kifaa cha mwanga mwekundu au mwanga wa sumaku umeme, kwa mfano hizi nishati ndogo katika mwili, hugundua nishati hiyo ya mwanga.

"Nishati hii itasimamia njia zinazoruhusu ufyonzaji wa glukosi, ambao umekatizwa kwa watu wanaosumbuliwa na kisukari cha aina ya pili," anasema Mtafiti Marie.

Anaendelea: "Changamoto yetu hapa ni kuonyesha kwa mwanga mwekundu. Tunaweza kurejesha njia hii ili kuboresha ufyonzaji wa glukosi na hivyo kupunguza uchochezi unaopatikana katika viungo vinavyolengwa na insulini."

**GHARAMA ZA UTAFITI**

Ni teknolojia inayopendekezwa na Marie itumike kwa maagizo na matibabu ya daktari, aki sisitiza "kwa sasa, tuko bado katika hatua ya majaribio...

Tuna majaribio mengi ya kufanya. Tuna marekebisho mengi ya kufanya ili tuweze kumruhusu mgonjwa kutibiwa."

Kwa sasa, Marie anaendelea kuboresha utafiti wake kwa kufanya majaribio kwenye mifano ya wanyama.

Ili kufikia bidhaa bora ya mwisho, mtafiti anahitaji kupitia hatua tatu zinazohitaji uwekezaji mkubwa wa muda, maarifa, na hasa rasilimali za kifedha na vifaa.

Hatua ya kwanza inatajwa ni kufanyia utafiti ndani ya glasi yenye mfanano na kiumbe hai, inafanywa kikamilifu katika maabara.

Hatua ya pili, ni majaribio kwa panya na ndicho kiwango amefikia wakati wa kuandika makala hiyo.

**AENDAKO SASA**

Kitaalamu inatajwa iwapo Marie atafanikiwa kutekeleza hatua hizo mbili kwa kutumia rasilimali chache alizo nazo, anahitaji fedha zaidi kuendelea na hatua ya mwisho.

"Utafiti unahitaji fedha nyingi... Kwa sasa, hatujaridhika na aina ya ufadhili tulionao, lakini tunajizatiti na kile tulichonacho," anasema, akibainisha dhamira yake, inabaki ni kutokana na uzoefu wake binafsi ulioelezwa awali.

Kwa tuzo hiyo kutoka kwa Taasisi ya L'Oréal-UNESCO, Marie anafurahia kwa kauli; "Tuna matumaini kupata ufadhili zaidi ili tuendelee na hatua ya majaribio ya kliniki."

**KUSHINDA VIKWAZO**

Katika Afrika ya Kusini mwa Sahara, wanawake wanawakilisha asilimia 31 tu ya watafiti wanapokea mishahara midogo na mara nyingi hawatambuliwi kama wenzao wa kiume.

"Changamoto ya kwanza tunayokutana nayo, ni ukosefu wa fedha hasa katika Afrika ya Kusini mwa Sahara, Magharibi mwa Afrika, katika nchi yangu," anasisitiza Dk. Chabi.

"Hivyo, natumai kweli kuwa naweza kuvuta umakini wa watu au taasisi zinazovutiwa na mada hii ili waweze kujitolea na kuniruhusu kuafiki ubora wangu ili kutoa bidhaa halisi inayofanya kazi."

La pili linatajwa, ni imani binafsi kulingana na mwanafunzi huyo wa sayansi za baiolojia, akiwa maelezo: "Nililazimika kufanya kazi sana na kujipa motisha ili niwe na imani na nafsi yangu na ninajijua kuwa, kadri ninavyotaka jambo fulani, najitahidi nikiwa na lengo la kulifikia."

"Sijakutana na ubaguzi mwingi, lakini haina maana hakuna ubaguzi...Kila wakati ninachukua kwa umakini ushauri kutoka kwa wazee ambaye huniambia kwamba hata kama nitajitahidi, nitahakikisha kila kitu kiko shwari bado nitakosolewa na hilo nisiweke akilini," anasema.

"Kwa falsafa hii, naendelea na utafiti wangu, bila kujali vikwazo vilivyopo," anahitimisha mtafiti Marie.

**AINA ZA KISUKARI**

- Aina ya Kisukari cha Kwanza; WHO inasema inatokana na uzalishaji mdogo wa insulini mwilini, hivyo inahitaji usambazaji wa nje wa insulini kwa mwili wa mgonjwa.

Dalili zake ni pamoja na kukojoa kila mara, kiu isiyokoma, njaa ya kila mara, kupungua uzito, matatizo ya kuona, na uchovu.

Aina ya Kisukari cha Pili; WHO inasema hii inatokana na uzalishaji mdogo wa insulini au mwili kushindwa kutumia insulini vizuri. Aina hiyo ya ugonjwa, ambayo awali ilikuwa inawaathiri watu wazima, WHO inasema imeenea kwa watoto wengi.

Dalili zake ni kama za aina ya kwanza, na husababishwa na uzito kupita kiasi na ukosefu wa mazoezi. Hii imeonekana kwa asilimia 95% ya watu waliogundulika na kisukari.

- Kisukari cha Ujauzito: Hali hiyo ya ki sukari ya juu mwilini hutokea kwa wajawazito na ina hatari kubwa ya matatizo wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua. "Watoto wao pia wako katika hatari kubwa ya kupata kisukari cha aina ya pili," anasema WHO.

- ***Kwa mujibu wa habari za BBC.***

## SAFARI YA DK. SAMIA KUSAMBAZA HUDUMA DHARURA HOSPITALI INAYOOKOA NUSU YA VIFO

**Inaendelea Uk. 14**

mwanzoni mwa mwaka jana, zikiwa ni jitihada za kusaidia kupata wataalamu mabingwa wa afya kwa fani tofauti, watakaotumika kujenga uwezo wa wataalamu wengine nchini katika vyuo vya mafunzo ya afya.

"Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuimarisha upatikanaji wa wataalamu wabobezi kwa ajili ya utoaji wa huduma za Kibingwa na Ubingwa Bobezi, kwa kuanzisha Dk. Samia 'Super Specilized Scholarships'.

"Hadi sasa jumla ya wataalam 1,211 wamepata mafunzo mbalimbali ya kibingwa na bobezi...jitihada hizo zitaimarisha upatikanaji wa huduma hizo za kibingwa bobezi ambazo zitawezesha nchi kunufaika na tiba utalii," inaelekezwa katika ripoti hiyo.

Zinatajwa nchi za kigeni wanufaika wa tiba utalii ni Comoro, Burundi, Malawi, Kenya, Congo DRC, Uganda na Zambia.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, safu ya wataalamu wanufaika mafunzo kati ya mwaka 2021 an 2024, wameongezeka kutoka 535 wa mwaka 2021 wakati Dk. Samia anaingia madarakani, hadi wataalamu 1,211 kwa mwaka wa sasa.

MAZINGIRA

## KILICHOSHINDIKANA MIAKA, GHAFLA KIMEWEZEKANA...

# Kutana na mradi unaotatua migogoro mipaka, misitu vijijini Handeni, Kilindi

## • Mageuzi; miradi maendeleo yachipua...

**Na Beatrice Philemon, aliyekuwa Handeni**

UNAPOZUNGUMZIA usimamizi shirikishi wa misitu, siyo wananchi wote katika wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, sasa wanaelewa faida ya usimamizi wa misitu, ikiwa ni zao la 'darasa misitu.'

Dhana usimamizi shirikishi wa misitu, ni mkakati wa kisera ulioanzishwa nchini, kuwahimiza wananchi katika mikoa mbalimbali, kusimamia na kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwenye ardhi za vijiji vyao.

Katika maeneo mengi nchini, mkakati huo umesaidia wananchi wengi wenye misitu ya hifadhi ya vijiji kujenga shule, zahanati, visima vya maji, wananchi kupata bima za afya, kujenga barabara, madarasa na miradi mingine kupitia usimamizi shirikishi wa misitu.

Ili wananchi waweze kunufaika na usimamizi shirikishi wa misitu kwenye ardhi za vijiji, Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa Kushirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) wameanzisha mradi wa kuleta suluhisho la Ujumuishaji wa Misitu na Nishati Endelevu ya Tungamotaka Tanzania (IFBEST), katika wilaya ya Handeni.

Lengo la mradi ni kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira, kwa kuboresha usimamizi endelevu wa misitu na uzalishaji endelevu wa nishati ya tungamotaka.

### MWENYEKITI MALIASILI

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili wa Kijiji cha Gendagenda, Ali Mikumi anasema, hadi sasa kupitia mradi wa IFBEST, wananchi wamefundishwa jinsi ya kusimamia na kuhifadhi msitu.

Anafafanua katika hilo, wanatenga hifadhi ya kijiji kwa ajili ya usimamizi shirikishi wa misitu, uzalishaji mkaa endelevu, matumizi ya GPS (mfumo wa utambuzi wa maeneo duniani unaotumia satelaiti) na jinsi ya kuanzisha vikundi vya mpango hisa.

"Kutokana na elimu tuliyoipata, tumefanikiwa kutenga msitu wa hifadhi ya kijiji wenye ukubwa wa hekta 4799.5 kwa ajili ya usimamizi shirikishi wa misitu na uzalishaji mkaa endelevu, kujua umuhimu wa kuhifadhi misitu na faida zake, kuanzisha vikundi vya mpango hisa na uzalishaji mkaa endelevu," anasema.

Anasema, ingawa wamepata elimu hiyo, kamati ya maliasili bado inahitaji kupata mafunzo ya kijeshi, ili kusimamia msitu vizuri, kupambana na wavamizi wanaoingia ndani ya msitu wa hifadhi ya kijiji kinyume na sheria kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo na uchomaji mkaa.

Pia, anataja kuna changamoto ya mipaka, hakuna 'beacon' (mawe yaliyopandwa ardhini kuonyesha mipaka ya eneo lililopimwa) hasa mpakani mwa msitu wa hifadhi ya kijiji, bado watu wanaingia ndani ya msitu wanachoma mkaa na mbao.

"Tunaomba Halmashauri ya Wilaya ya Handeni itusaidie kuweka 'beacon' kwenye mipaka ya kijiji," anasema.

Anasema, wanaomba kuwekewa 'beacon', kwa sababu wanakijiji watokao Mtango, Kwakibuyu na Mseko bado wanaendelea kuingia kwenye msitu kukata miti kwa ajili ya uchomaji mkaa.

Pia, wanaomba vifaa kwa ajili ya kufanya doria msituni, katika hifadhi ya kijijini Gendagenda, zikiwamo sare za Wajumbe wa Kamati ya Maliasili, buti za kutembelea porini, pikipiki na 'GPS'.



Wataalamu wa ardhi katika halmashauri za wilaya ya Handeni na Pangani, wakipitia matangazo ya serikali na miongozo, kabla ya kwenda kutafsiri kwa wananchi wake, ikiwa ni sehemu ya utatuzi wa migogoro yao. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

### MNUFAIKA MRADI

Zaituni Omary, ni miongoni mwa wanawake katika kijiji cha Gendagenda, Handeni walionufaika na mradi wa IFBEST.

"Tunashukuru TFCG na MJUMITA kuleta mradi wa IFBEST katika kijiji chetu, kinamama tunafanya kazi bila ya woga, tunajiamini, mradi huu umetuthamini, tunafanya kazi kwa pamoja kwenda kufanya 'patrol' (doria) msituni kwa kushirikiana na wanaume, tofauti na miaka ya nyuma," anasema.

### OFISA MTENDAJI KIJIJI CHA GENDAGENDA

Musa Kihumbi, ni Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Gendagenda, anasema mradi huo wa IFBEST, umesaidia kuondoa changamoto za wakulima na wafugaji katika kijiji hicho, baada ya kufahamu mipaka kati ya vijiji iliko.

"Labla ya mradi hali ya msitu ilikuwa mbaya, lakini tangu mradi uanze, msitu wetu umekuwa mzuri na sasa hivi tutaanza kufanya biashara ya hewa ukaa, uchomaji mkaa endelevu na pia hivi sasa tunatunza mazingira na msitu wetu ili tunufaike na hewa ukaa kwa kuuza 'carbon' (ukaa)," anasema.

Anaeleza kushukuru ufadhili wa kimataifa, kupitia Wizara ya Fedha, umewezesha kuwapo mradi huo kijijini, ikifanikishwa kupitia mpango wa matumizi ardhi.

"Hapo mwanzo katika kijiji chetu hapakuwa na msitu wa hifadhi, watu walikuwa wanaingia kwenye msitu wanakata miti ovyo, kuchoma mkaa, mbao na mifugo, lakini baada ya kuja radi tumeweza kutenga msitu wa hifadhi ya kijiji ambao tunauhifadhi kisheria," anasema.



Sehemu ya mandhari ya Wilaya ya Handeni, iliyozingirwa na misitu ya asili. **PICHA: MTANDAO**

### WENYEVITI MIRADI

Bakari Athuman, ni Mwenyekiti wa Mtandao wa MJUMIKWEKIGE, unaounganisha vijiji vitatu; Gendagenda, Kwedihawala na Kitumbi, anawashukuru wakuu wa wilaya za Pangani na Handeni na Mpima Ardhi Mkoa, kwa kuwasaidia kutatua mgogoro kati ya kijiji cha Gendagenda na Mkalamo.

Anataja bado kuna eneo lingine la mgogoro wa mipaka kati ya vijiji vya Gendagenda na Mtango; Gendagenda na Kwa Kibuyu; Gendagenda na Mbulizaga; pia Gendagenda na Mseko.

### WITO KWA WADAU

"Tunamwomba Kamishna wa Ardhi Mkoa, Ofisa Ardhi kutoka wilaya za Pangani na Handeni, waje kumalizia zoezi la kuainisha mipaka ya vijiji, kwa sababu zoezi la kuainisha mipaka walililisimamisha, wakisema mpaka Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uishe ndiyo watarudi tena.

"Sasa uchaguzi umeisha, tunawaomba waje kumalizia zoezi hili, ili tuweze kusimamia vizuri msitu wetu wa hifadhi ya kijiji na hatimaye tuweze kunufaika na rasilimali za misitu iliyopo katika kijiji chetu kwa maendeleo ya kijiji na wananchi kwa ujumla," anasema Bakari Athuman, Mwenyekiti wa Mtandao unaounganisha vijiji vitatu.

### DIWANI KATA MGAMBO

Hamis Mwang'ona, ni Di-

Inaendelea Uk. 14

AFYA

# Pata simulizi ya vizazi na sifa zao; vilivyopita, vya sasa, hadi vijavyo

**Na Christina Mwakangale**

KILA kizazi kina jina lake. Kwa mujibu wa wanasayansi duniani, vizazi hupewa majina, ili kubainisha watu waliozaliwa katika kipindi fulani cha wakati, wakiwa na ushawishi wa kitamaduni unaoathiri kila kizazi.

Majina ya vizazi yanategemea mwelekeo wa kijamii wa kihistoria na yanaweza kutofautiana kulingana na nchi.

Hivi karibuni kumetajwa kuwapo kizazi kinachoitwa cha 'Gen Z' kinacholeta taswira mpya mitandaoni, kutokana na watu walio wengi kutofahamu kwa undani kuhusu kundi hilo na majina ya vizazi hivyo.

Kundi la kijamii la 'Gen Z 'wa Kenya walivuma hasa mwaka jana, baada ya kuwapo maandamano kuipinga serikali ya Rais William Ruto.

Kupitia mtazamo huo, umfanyiwa kazi Nipashe, ikikusanya taarifa mbalimbali za habari kimataifa, kukiwapo aina ya vizazi, kila kimoja kikiwa na miaka pia zama zake.

Baadhi ya mifano ya majina ya vizazi na matukio yaliyoathiri kila kizazi:

Kwanza; ni kizazi cha 'The Lost Generation': Hiki ni kizazi cha waliozaliwa 1883-1900. Kizazi hicho kilishuhudia Vita vya Kwanza vya Dunia na uhamaji mkubwa duniani.

Pili; ni kizazi cha 'The Greatest Generation': Hao waliozaliwa kati ya miaka 1901-1924, ambao walikulia kilikulia wakati unaoitwa 'Great Depression' (Unyogovu mkubwa) na pengine walishiriki katika Vita vya Pili vya Dunia.

Kizazi cha tatu; ni 'The Silent Generation': Hicho ni kizazi cha waliozaliwa kati ya miaka 1925 hadi 1945, ambacho pia kilikulia katika kipindi cha utoto baada ya vita.

**BAADA VITA KUU**

Kwa mtiririko wa wanasayansi,



Picha tofauti za makundi mawili kijamii, yanaangukia vizazi tofauti kwa mujibu wa wataalamu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

kizazi cha nne wanakiita 'Baby Boomers', ambaoni ni watu waliozaliwa kati ya mwaka 1946 na 1964.

Inaelezwa wakati huo, kulikuwapo ongezeko kubwa la uzazi katikati ya karne ya 20. Hicho ni kizazi cha demografia kwa lugha nyingine, kinachokuja baada ya 'Silent Generation' na kabla ya 'Generation X.'

Inaelezwa kwamba neno "baby boom" linarejelea kipindi cha ongezeko kubwa la uzazi katika eneo fulani la kijiografia.

'Baby Boom', uliofanyika katikati ya karne ya 20 unadhaniwa kuanza baada ya Vita vya Pili vya Dunia na kumalizika katika miaka ya 1960.

Kizazi cha Tano; ni 'Generation X au Gen X, ni kundi la demografia la watu waliozaliwa kuanzia katikati ya miaka ya 1960 na mwishoni mwa miaka ya 1970.

Kwa ujumla, kundi hilo linafafanuliwa kipindi cha 1965 hadi 1980. Ni kizazi kilichofuata Baby Boomers na kabla ya Millennials.

Kizazi cha Sita; ni 'Millennials'. Hicho ni kizazi cha watu waliozaliwa kati ya mwanzoni mwa miaka ya 1980 na katikati ya miaka ya 1990, ingawa miaka halisi ya kuzaliwa inaweza kutofautiana.

Kwa mujibu wa Kituo cha Utafiti cha Pew, Millennials, kuna watu waliozaliwa kati ya miaka 1981 na 1996. Hata hivyo, watafiti wengine hujumuisha watu waliozaliwa mapema kama 1980 au kama vile 2004.

Kizazi cha saba ni 'Generation Z' au Gen Z, ni idadi ya watu waliozaliwa kati ya katikati hadi mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa 2010.

Pia zinajulikana kama 'Zoomers' na ni kizazi baada ya Milenia na kabla ya Kizazi Alpha.

Kizazi cha Nane; ni 'Generation Alpha' ni kizazi cha watu waliozaliwa baada ya mwaka 2010 na kabla ya katikati ya miaka ya 2020.

Hiki ndicho kizazi cha kwanza kuzaliwa kabisa katika karne ya 21 na kinajulikana kwa ufanisi wake katika teknolojia, kujitegemea na kuwa na roho ya ujasiriamali.

Kizazi cha Tisa; ni kilichoanza mwaka huu. 'Gen Beta'; Hicho ni kizazi cha watu waliozaliwa kati ya 2025 na hadi ifikapo 2039, wanatajwa wataotwa 'Watoto wa Milennia Wachanga na Gen Z.

Ubashiri McCrindle inatabiri kuwa ifikapo 2035, watakuwa ni asilimia 16 ya idadi ya watu duniani.

Wengi pia wataishi na kuiona karne mpya ya 22. Watoto hao pia watakuwa wanajua tu dunia ilivyo, baada ya janga la Uviko 19.

Watajivunia kwa kuona maneno ya zamani na wataomba tuzime muziki wa zamani.

Pia, watoto hao wa Gen Beta, wanatajwa watalelewa katika enzi ya ujumuishaji wa kiteknolojia pamoja na Gen Alpha.

McCrindle inafafanua " hiyo ndiyo sababu ya kuhamia kwenye Alfabeti ya Kigiriki mwaka 2010, sio vizazi vipya tu, bali vya kwanza, vitakavyoshinikizwa na dunia tofauti kabisa.

"Kwa Generation Beta, ulimwengu wa kidijitali na wa kimwili utakuwa na uhusiano wa karibu," McCrindle inafafanua kwenye tovuti yake.

"Ingawa Generation Alpha, imeona kuongezeka kwa teknolojia za 'smart' na akili bandia (AI), Generation Beta itaishi katika enzi.

"AI na automatiska zimejumuishwa kikamilifu katika maisha ya kila siku kutoka kwa elimu na sehemu za kazi hadi huduma za afya na burudani."

Aidha, inaelezwa simu za mkononi zilivyounda kizazi cha 'The Anxious Generation' ya watoto.

Juhudi za kuwaondoa watoto kwenye skrini na kuwapeleka kwenye dunia, halisi zilipata nguvu zaidi mwaka huu, kupitia kitabu kinachouza vizuri The Anxious Generation.

Mwandishi na Mwanasosholojia, Jonathan Haidt, anasema kwa mwenyeji wa CBC The Current, Matt Galloway, kuhusu utafiti wake na jinsi simu za mkononi zilivyobadilisha fahamu na uzoefu wa binadamu.

**CHANGAMOTO ZA VIZAZI**

Taasisi ya Afya ya Umma, inasema kuwa wazazi wa leo wanakutana na changamoto za kipekee zinazoweza kuathiri afya zao za akili.

Wazazi kutoka kwa vizazi vya zamani wanasema kuwa kulea watoto imekuwa na itakuwa changamoto kila wakati.

"Wakati wazazi wengi wa milennia walitumia mitandao ya kijamii kuandika maisha ya watoto wao, 'Generation Z' inajua zaidi kuhusu faida na changamoto zinazokuja na matumizi ya mitandao ya kijamii kutoka utoto," McCrindle inaeleza.



# Kutana na mradi unaotatua migogoro mipaka, misitu vijijini Handeni, Kilindi

**Inatoka Uk. 13**

wani Kata ya Mgambo, anasema hadi sasa wamefanikiwa kwenda wilaya ya Tanganyika katika mkoa wa Katavi kujifunza namna kuhifadhi ya misitu, kujenga shule, pia zahanati kupitia uhifadhi wa misitu.

"Kama diwani, nipo tayari kuhakikisha misitu inaendelezwa katika kata yangu, ili wananchi waweze kunufaika na rasilimali za misitu,' anasema Mwang'obna.

Augustino Gervas, Ofisa Usimamizi Shirikishi wa Misitu, anaahidi mapato yatakayopatikana kutokana na usimamizi shirikishi wa misitu katika kijiji cha Gendagenda zitatumika kufanya doria msituni, shghuli za maendeleo ya kijiji, kununua sare za kamati ya maliasili na mafunzo zaidi kwa ajili ya doria.

"Naishukuru mradi wa IFEBEST kwa sababu TFCG na MJUMITA walitoa wataalamu wawili, yaani Ofisa Ardhi kwenda kutatua migogoro wa mipaka, kati ya wilaya ya Pangani na Handeni," anasema.

Anasema kabla ya mradi, kijiji cha Gendagenda kilikuwa na msitu, lakini ulikuwa haujatengwa kama wa hifadhi ya kijiji.

Hadi sasa wilaya ya Handeni imefanikiwa kutenga hekta 1,060 za misitu kwa ajili ya uzalishaji wa mkaa endelevu, katika vijiji vya Gendagenda na Mkalamo.

**OFISA MALIASILI**

Napoleon Mlowe, ni Ofisa Maliasili Wilaya ya Handeni, ana maelezo yake kuwa: "Tunaishukuru MJUMITA na TFCG kuja katika wilaya yetu, mradi huu wa IFBEST unaotekelezwa katika vijiji vitatu; Kijiji cha Kwa Msisi, Gendagenda na Mkalamo na umelenga zaidi katika misitu ya vijiji."

Anasema, kupitia mradi, wamepewa elimu kuhusu uhifadhi wa msitu na namna wanavyoweza kunufaika na msitu, mazao ya msitu na elimu ya utawala bora.

Mlowe anasema mradi umesababadilisha jamii zote, kiuchumi, kijamii na matokeo kubwa ya wanalohitaji ni vijiji wapate mapato kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Pia, kupitia mradi huo, anaahidi wananchi wataanza kujihusisha na biashara ya hewa ukaa kupitia uhifadhi wa misitu.

Lingine, anaahidi kupambana na mabadiliko ya tabianchi, pia jamii kunufaika na mapato ya rasilimali za misitu.

"Kama Wilaya ya Handeni, tumetenga shilingi milioni 15 kusaidia shughuli za uhifadhi wa misitu ya vijiji," anasema Mlowe.

Pia, anataja vikundi vya mpango hisa ambavyo vimeanzishwa, wilaya ya Handeni itaelekeza kiasi cha fedha kielekezwe kwenye vikundi hivyo.

Dhamira anataja ni kusaidia vikundi vinavyofanya shughuli za uhifadhi wa mazingira, ikiwamo misitu waweze kupata mkopo wa asilimia 10.

Mapato ya ndani yataendelea kupangwa kwenye shughuli za uhifadhi wa misitu, hadi sasa wilaya ya Handeni ina vijiji 91na ina misitu ya vijiji 32,000.

# Dendego awacharukia maofisa ugani

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amewaamuru maofisa ugani kwenda kuishi vijijini katika maeneo ya kazi waliyopangiwa na serikali badala ya kuzurura mjini.

Dendego alisema kuanzia sasa kila ofisa ugani ahakikishe anakaa kwenye kituo chake cha kazi na kuishi huko badala ya kuwa mjini, la sivyo watawajibishwa kwa mujibu wa sheria.

"Nisiwaone hapa mjini, nataka kuwakuta wote kwenye vituo vyenu na kuishi huko huko, kule mlikopangiwa," alisisitiza mkuu huyo wa mkoa.

Alisema haiwezekani kila siku ofisa ugani anasafiri kutoka mjini kwenda kijijini alikopangiwa kazi, hali hiyo kamwe haikubaliki mkoani kwake.

Dendego, alisema haifai kwa maofisa au wakuu wa idara kukaa mjini wakati wamepangiwa kufanya kazi vijijini kwa kuwa wanazorotesha utendaji kazi.

Vilevile, aliwataka maofisa hao kuacha kuendelea kufanya kazi kwa mazoea na kuzingatia maadili ya kazi.

Aliwakumbusha umuhimu wa kutekeleza majukumu yao ipasavyo, ikiwemo kuvaa mavazi rasmi ya kazi yanayojulikana kama 'kombati' ili watambulike zaidi kwa wananchi na wakulima vijijini.

Alisema uwekezaji wa serikali katika sekta ya kilimo hautakuwa na tija bila ya uwepo wa wataalamu wa kutosha na wenye nidhamu.

Alisema maofisa hao wanapaswa kuzingatia maadili ya kazi ili kuongeza tija katika kilimo na kuboresha uchumi wa wakulima na wananchi.

Kwa upande mwingine, Dendego alikemea matumizi mabaya ya vifaa vya kazi vinavyotolewa na serikali yanayofanywa na baadhi ya maofisa hao ugani.

Alisema baadhi ya wanatumia vishikwambi na pikipiki kwa shughuli binafsi na kukwamisha usimamizi wa shughuli za kilimo kwa wakulima vijijini.

Aliwataka maafisa hao kutumia vifaa hivyo kwa kufuatilia sera za kilimo na masuala mengine muhimu.

# Watoto 18,000 kujiunga awali

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WILAYA ya Dodoma inatarajia kuandikisha watoto 18,252 kwa ajili ya kujiunga na darasa la awali mwaka huu.

Takwimu hizo zilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya hiyo, Jabir Shekimweri wakati akizungumzia uhamasishaji wazazi, walezi na walimu kuandikisha watoto watakaonza masomo muhula wa masomo kwa mwaka huu unaotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Shekimweri, alisema idadi ya watoto hao wanaotarajia kujiunga na darasa hilo la awali, ni sawa na asilimia 38.

Alisema wakati shule zikitarajiwa kufunguliwa nchini wiki ijayo, wilaya hiyo imeandikisha watoto 6,893 kwa ajili ya kuanza masomo mwaka huu.

Alisema kutokana na hali hiyo wazazi na walezi wanatakiwa kuweka kipaumbele kwa kuwekeza kwenye elimu kwa watoto ili kuwasaidia kutimiza ndoto zao kwa baadaye.

"Wazazi, walezi, ndugu, jamaa na marafiki ni wajibu wetu katika kutekeleza sera ya elimu, kusimamia haki za msingi za watoto hususani haki ya kupata elimu na kujumuika, kuchukua hatua ya kuandikisha kwa wale wanaoanza madarasa ya awali na darasa la kwanza," alisema mkuu huyo wa wilaya.

Aliipongeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kuhakikisha uandikishaji wa mwaka uliopita unafikia asilimia 98 kwa darasa la awali.

"Nichukue nafasi hii kuipongeza Jiji la Dodoma, pamoja na idara ya elimu ya msingi na wataalamu wote kwa kazi nzuri waliyoifanya msimu wa uandikishaji uliokwisha kwa darasa la awali," alisema.

Kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia shuleni, aliwataka walimu kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kuhamasisha ili kutunza mazingira.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amehamasisha na kusema kuwa kwenye mikusanyiko ya watu zaidi ya 100 wahamie katika matumizi ya nishati safi ya kupikia kufikia tarehe 31 Desemba, 2024. Kwa hiyo, niombe shule zote kukaguliwa na wengine walikuwa kwenye hatua ya mwisho ya kufunga mifumo hiyo.

"Nipende kusisitiza tusikute shule yenye watu zaidi ya 100 bado wanatumia nishati chafu ya kupikia," alisisitiza Shekimweri.

Hata hivyo, aliwataka wakuu wa shule, walimu, vilabu vya mazingira na vyuo vikuu kuendeleza kampeni ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani msimu huu wa mvua kwa kupanda miti ya matunda, vivuli na bustani ili kuwajengea watoto tabia ya kupanda miti.



Katibu Mkuu wa Shirika la Kutetea Haki za Abiria nchini (SHAKUHA), Hashim Ramadhan (kulia), akijadiliana na viongozi wa kikosi cha usalama barabarani kuhusu kutatua changamoto zinazowakumba abiria jijini Dodoma juzi. Katikati ni Mkuu wa Trafiki Dodoma, SSP Yusuph Kamotta na Mkuu wa Trafiki wa Wilaya ya Dodoma, ASP Maison Matiko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri yaagiza uvuvi haramu udhibitiwe

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Singida mkoani imewaagiza wenyeviti, watendaji wa vijiji na kata kudhibiti uvuvi haramu kwenye mabwawa yaliyopo maeneo yao ili kunusuru mazalia ya samaki na kuongeza mapato ya serikali.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Elia Digha, alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao cha wadau wa uvuvi kilichofanyika mjini hapa.

Digha, alisema wenyeviti na watendaji hao wanatakiwa kuhakikisha wanawatambua viongozi wa wavuvi, wavuvi kwa kuwasajili na kuwafahamu wageni wanaoingia katika vijiji vyao kwa shughuli za uvuvi ili iwe rahisi kudhibiti uhalifu kwa kuwakamata watuhumiwa.

" Kuna wavuvi wageni ambao wanaenda kila mahali, watu kama hawa wanaofanya mzunguko mkubwa ni lazima tujiridhishe kwa kutambua uongozi wa wavuvi, tukawajua wavuvi wote na usajili wao wote, maana wapo wasio na nia njema," alisema.

Alisema watu wa aina hiyo wanafanya uhalifu sehemu nyingine na kwenda kujificha kwenye maeneo ya uvuvi ya halmashauri hiyo.

"Anapokuja mgeni tujue huyu ni mgeni kaja, tujuane ili twende vizuri," alisema.

Katika kikao hicho wavuvi na viongozi wa wavuvi kutoka vijiji vyenye mabwawa hayo waliwasilisha changamoto zao na kupatiwa majibu ili kuongeza ufanisi wa kazi zao za uvuvi na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na samaki.

Vilevile viongozi walisisitizwa kila mmoja kutimiza wajibu kuhakikisha ukusanyaji wa mapato ya samaki unaongezeka.

Kwa upande wawavuvi, walihimizwa kuhakikishawanavaa makoti ya uokozi kwa usalama wao wawapo katika shughuli zao, kuunda vikundi vya wavuvi vinavyokopesheka, kuacha matumizi ya nyavu haramu kuvulia samaki kwa lengo la kulinda mazalia ya samaki. Maofisa wa serikali, nao walitakiwa kutengeneza urafiki na wavuvi ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya samaki.





# 260 wakumbwa kipindupindu Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UGONJWA wa kipindupindu umeendelea kulitesa Jiji la Mbeya baada ya zaidi ya watu 260 kubainika kuugua mwanzoni mwa wiki hiyo.

Mganga Mkuu wa Jiji hilo, Dk. Yesaya Mwasubila, alitoa takwimu hizo kwenye kikao kazi cha kujadili mikakati ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko jijini hapa.

Dk. Mwasubila, alisema katika kikao hicho kuwa idadi kubwa ya wagonjwa hao ni wanaume kwa kile kinachodaiwa kusababishwa na mfumo wa utafutaji.

Alisema kati ya kata 36 za jiji hilo, 10 zimebainika kuwa hazina wagonjwa wa kipindupindu.

Aliitaja Ilemi kuwa ndiyo kata inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa katika halmashauri hiyo.

Mwasubila, alisema uchunguzi wa wataalamu wa afya umebaini kuwa chanzo cha mlipuko wa ugonjwa huo ni matumizi ya maji machafu kwa baadhi ya wakazi wa jiji hilo.

Alisema kati ya wagonjwa 261 waliohudumiwa kwenye vituo vya kutibu kipindupindu, 193 ni wanaume na 12 ni watoto chini ya miaka mitano.

Alisema wametenga vituo vitatu vya kuwahudumia wagonjwa wa kipindupindu katika Hospitali ya Wilaya ya Igawilo, Kituo cha Afya Iganzo na Kituo cha Afya Ndanyela.

"Pamoja na idadi ya wagonjwa tuliowabaini na kuwahudumia, bado kuna wagonjwa mitaani ambao wanajificha wakiogopa kuwekwa kizuizini, hao ndio wanasababisha tatizo hili kuendelea kusumbua, tunawaomba sana tusaidiane kutoa elimu," alisema Dk. Mwasubila.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sisimba, Jumapili Mwasenga, alisema moja ya visababishi vya mlipuko wa ugonjwa huo ni kufumuka kwa mifuniko ya majitaka na kuzagaa mitaani.

Mwasega, aliiomba Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya UWSA) kudhibiti chemba za maji taka ikiwa ni pamoja na kutibu maji kwa kutumia dawa maalumu za kuua vimelea vya magonjwa.

Alisema watendaji wa mamlaka hiyo wamekuwa wakishughulikia chemba hizo kwenye maeneo yaliyoathirika pekee jambo ambalo alidai linaweza likasababisha mlipuko wa ugonjwa huo kuendelea.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini, Dk. Salvatory Mhando, aliwaomba watendaji wa mitaa na kata kufuatilia mazingira ya vilabu vya pombe za kienyeji kwani yanaweza kuwa chanzo cha kuenea kwa ugonjwa.

Alisema maandalizi ya pombe hizo mara nyingi huwa ni machafu na baadhi ya vyakula vinavyoandaliwa kwenye maeneo hayo si salama kwa afya za wananchi.

Aliiomba serikali kuwatumia wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu jijini hapa kutoa elimu kwa wananchi ili kuhakikisha ugonjwa huo unadhibitiwa haraka.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliagiza kila kata kuunda timu ya kutoa elimu kwa wananchi ambayo itawahusisha wananchi, viongozi wa dini na wa mila.

Malisa, aliwataka wadau wa afya na mazingira ndani ya jiji hilo kushiriki vita dhidi ya ugonjwa huo ili ndani ya muda mfupi udhibitiwe na kuokoa maisha ya wananchi.

Ugonjwa huo ulianza kulipuka jijini hapa katikati mwa Desemba mwaka jana.



Baadhi ya wadau wa afya katika Jiji la Mbeya wakishiriki kikao kazi cha kujadili mikakati ya kudhibiti kipindupindu kilichofanyika juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**



## Mwanyika akabidhi 'ambulance' kwa msisitizo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MBUNGE wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika, amesisitiza gari la kubebea wagonjwa lililotolewa na serikali litumike kwa malengo yaliyokusudiwa kuokoa maisha kwa wanaohitaji huduma za dharura.

Mwanyika alitoa kauli hiyo juzi wakati akikabidhi gari hilo (ambulance) katika Kituo cha Afya Ihalula.

Alisema hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za serikali za katika kuboresha huduma za afya inapotokea dharura ma utekelezaji wa ahadi alizozitoa kwa wananchi.

"Tangu ziara yangu ya kwanza nilipofika hapa, moja ya changamoto mlizoniambia haswa akina mama ni gari la wagonjwa wa dharura na niliitoa ahadi, diwani wenu amekuwa akinikumbusha mara kwa mara na leo ninafurahi kuwa ahadi imetimia," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete alisisitiza gari hilo litunzwe na kuwahudumia wananchi kwa muda mrefu.

Mganga Mfawidhi Kituo hicho, Dk. Happyness Kwilasa, alisema bado wanakabiliwa na upungufu wa watumishi hususani mtaalamu wa mionzi na nyumba za watumishi.

Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Jabil Juma, alisema halmashauri yao imepata magari matano ya wagonjwa wa dharura kwenye vituo vya afya vinne na moja hospitali.

## Dk.Tulia amkomboa yatima kuponda kokoto, kujisomesha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ameahidi kumsomesha mtoto Yohana Japhet (14) ambaye amekuwa akiishi kwa kubonda kokoto na kuuza ili apate fedha kwa ajili ya kununua chakula na mahitaji ya shule baada ya kufiwa na wazazi wake.

Dk. Tulia alitoa ahadi hiyo jana alipotembelea familia ya mtoto huyo katika Mtaa wa Ituha, Kata ya Ilomba jijini Mbeya ambako amekuwa akiishi na bibi wa kufikia.

Alisema atamhamisha mtoto huyo kutoka kwa bibi yake huyo na kuishi naye nyumbani kwake ilia some akiwa chini ya uangalizi wake.

Alisema akifaulu darasa la saba atamsomesha kuanzia kidato cha kwanza mpaka chuo kikuu.

Tulia, alisema mtoto huyo ni miongoni mwa watoto walionyesha juhudi za kutafuta maisha licha ya kuwa na umri mdogo.

"Tutamhamisha shule anayosoma, nitakaa naye nyumbani ili alelewe na kusomeshwa na Taasisi ya Tulia Trust, tutahakikisha anasoma mpaka chuo kikuu," alisisitiza Dk. Tulia ambaye pia ni Mbunge wa Mbeya Mjini (CCM).

Hata hivyo Dk. Tulia alimpatia bibi aliyekuwa anamlea mtoto huyo msaada wa chakula kilo 40 za mchele, nguo na blanketi kwa lengo la kumsaidia kuendesha maisha baada ya kumchukua mjukuu wake aliyekuwa anamlea.

## Madaktari bingwa macho wapiga kambi Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MADAKTARI bingwa wa macho wa Hospitali ya Dk.Agarwals Tawi la Mwanza wanatarajia kutoa huduma ya matibabu ya macho bure kwa wakazi mkoani hapa kesho.

Hayo yalibianishwa juzi na Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Faustine Mlyutu wakati akizungumza na waandishi wa habari kuujulisha umma juu ya huduma hiyo itakayotolewa na madaktari hao katika Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga.

Dk. Mlyutu, alisema wakazi hao wanatakiwa kufikia hospitalini hapo kujiandikisha, kufanyiwa uchunguzi wa afya ya macho na kupata matibabu bure.

"Huduma hii ni fursa kwa wananchi wa Shinyanga, wajitokeze kwa wingi kujiandikisha waje kupata tiba, na hawa ni watalaamu wa macho na wanapandikiza hadi mboni ya jicho," alisisitiza Mlyutu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Pierina Mwaluko, alisema ujio wa madaktari hao hospitalini hapo ni fursa kubwa kwa wakazi hao kutatua matatizo yao ya macho.

Dk .Agarwals Mwanza, alisema wanatoa huduma hiyo bure baada ya kubaini idadi kubwa ya wakazi wa Kanda ya Ziwa wanakabiliwa na tatizo la macho.

Babu, alitaja huduma watakazotoa kuwa ni pamoja na kupima uoni hafifu, presha ya macho, mtoto wa jicho na kupandikiza mboni ya jicho.



## SMZ yazihakikishia taasisi maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduara, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) itahakikisha taasisi zake zinapiga hatua kwa maendeleo na kukidhi mahitaji ya sasa.

Kaduara alitoa kauli hiyo jana wakati wa akiweka jiwe la msingi la Ofisi za Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar, lililopo Tunguu viswani hapa ikiwa ni Maadhimisho ya Miaka ya 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema ujenzi wa ofisi hiyo ukikamilika, itasaidia kurahisisha kazi, kuipatia serikali mapato na kuondoa changamoto mbalimbali ikiwemo kuchapisha magazeti kampuni binafsi.

Kaduara, alisema ni vema waandishi wa habari kuzingatia maadili na uzalendo wa nchi yao na kutumia kalamu zao vizuri kuielimisha jamii umuhimu wa kudumisha amani na utulivu.

Vilevilem, aliwataka waandishi wa habari kujikita zaidi kwa wananchi wa vijijini ili kuibua changamoto zinazowakabili na serikali kuzipatia ufumbuzi.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmuod, alisema mkoa huo umepiga hatua kwa maendeleo.

Mahmuod, alisema jumla ya miradi 17, imeziduliwa katika maadhimisho hayo ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Hamad Rajab alisema hadi sasa ujenzi wa mradi huo ambao umefikia asilimia 50 unatarajiwa kukamilika Septemba, mwaka huu.

Mradi huo hadi kukamilika, unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. Bilioni nane na kuwa na huduma zote muhimu, ikiwamo kiwanda cha uchapaji.

**Alisema ujenzi wa ofisi hiyo ukikamilika, itasaidia kurahisisha kazi, kuipatia serikali mapato na kuondoa changamoto mbalimbali ikiwemo kuchapisha magazeti kampuni binafsi**

# Wanachi Pemba kuuziwa vyakula kwa bei chee

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali inajipanga kupunguza gharama za bei za vyakula katika Kisiwa cha Pemba na kuuzwa kwa wananchi kwa gharama nafuu.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo wakati akizindua ghala lililoko Gando Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba linalomilikiwa na Kampuni ya Yasser Provision kwa ajili ya kuhifadhi chakula.

Alisema serikali inalenga kuwapunguzia mzigo wa gharama wafanyabiashara wanaoingiza vyakula nchini, wananchi kwa kuuziwa kwa bei nafuu na visiwa hivyo kuwa na ushuru maalum kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Alisema mpango wa kuifungua Pemba kiuchumi una dhamira thabiti ya kuhakikisha bei za bidhaa muhimu zinashuka na kutoa unafuu wa maisha kwa wananchi.

Alitaja ujenzi wa bandari za Mkoani, Shumba Mjini na Wete ambao utaanza hivi karibuni kuwa ni miongoni mwa hatua



muhimu ya kuwawezesha wafanyabishara kuingiza bidhaa zao moja kwa moja Pemba na kupunguza gharama za mzunguko wa usafirishaji.

Dk. Mwinyi alipongeza kampuni hiyo kwa ujenzi wa ghala hilo ili kusaidia kuhifadhi vyakula na kuahidi Serikali kuendelea kumuunga mkono mfanyabiashara huyo kwa kuhakikisha mzigo yake inashushwa Kaskazini Pemba.

Alisema serikali inajipanga kwa ujenzi wa maghala mengine ili kuwa na uhakika wa chakula visiwani hapa.

Mmiliki wa ghala hilo, Adil Yakoub Sadik, alisema lina uwezo wa kuhifadhi bidhaa mbalimbali bila ya athari yoyote.



Mwonekano wa Shule ya Sekondari Misufini iliyoko Bumbwini, Zanzibar baada ya kufunguliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan jana. **PICHA: IKULU**

# TIRA yatoa mamilioni sherehe za Mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, ameipongeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kutoa mchango wao kwa ajili ya sherehe za Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Abdullah alitoa pongezi hizo jana ofisini kwake Vuga baada ya Uongozi wa Mamlaka ya TIRA kukabidhi mfano wa hundi ya Shilingi milioni 321 kuchangia sherehe zitakazofanyika mwishoni mwa wiki hii visiwani hapa.

Alisema fedha hizo zilizotolewa TIRA zitasaidia kwa kiasi kikubwa kufanikisha sherehe hizo katika Uwanja wa Gombani kisiwani Pemba.

Alisema kampuni mbalimbali zinaendelea kuwekeza Zanzibar na kutoa fursa kwa TIRA kushirikiana na kuhakikisha wanakata Bima stahiki kwa ulinzi wa mali zao.

Alizishukuru kampuni za bima kwa kuendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na viongozi wakuu wa nchi kuwaletea maendeleo wananchi.

Aliwahakikishia TIRA kuwa serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa sekta binafsi katika uwekezaji.

Akikabidhi mfano wa hundi hiyo, Naibu Kamishna wa TIRA Zanzibar, Khadija Issa Said, alisema wamefarijika kukamilisha ahadi waliyoitoa kufanikisha sherehe hizo.

Khadija, alisema TIRA itaendelea kushirikiana na serikali katika kufanikisha utekelezaji wa miradi ya za maendeleo katika jamii.

Aliishukuru Serikali ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwapatia ushirkiano mkubwa katika utekelezaji wa kazi za mamlaka hiyo na kuwapa msukumo wa kufanya kazi kwa juhudi na uzalendo ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Umoja wa Makampuni ya Bima Tanzania ambaye ni Mkurugenzi wa Bima CRDB, Nelson Mnzava, alisema utaratibu huo wa kushiriki katika Mapinduzi utakuwa endelevu kwa kila mwaka kadiri hali itakavyoruhusu.

Mnzava, alitaka serikali kuwasaidia katika kuzishajihisha taasisi za serikali, taasisi binafsi na kampuni kujenga tabia ya kukata bima ili kuziweka katika mazingira salama.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MICKDAD LUKANDA EZEKIEL** anatangaza kupotea kwa Cheti cha Kidato cha Nne chenye Index namba **S.3283/0076** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari NYAKASUNGWA Mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi : **KR/RB/1811/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODWIN SILVANO CHIGANGWE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye INDEX NAMBA **S2463-0025** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **HEMBAHEMBA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/CHA/1318/2025.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**GEORGE GEBRA MSUYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S.0544-0078** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MKUU SECONDARY SCHOOL** mwaka 1999 , Cheti cha kidato cha sita chenye index No. **S.0142-0527** Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia GALANOS SECONDARY SCHOOL mwaka 2002. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/6659/2025**

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHALILA MUSA SAIDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye INDEX NAMBA **S3421/0041/2022** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **LUKIMWA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2022. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **CONTROL NO. 9910843291202**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAPPINESS JOACHIM MSANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Toyota IST yenye usajili namba **T 277 DAG,** CHASSIS NAMBA: **NCPE00033423** na ENGINE NAMBA: **2N2239E35.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu. POLISI TAARIFA: **PHQ/KAG/KAR/18896/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GASTO MATHEW MWACHA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Spacio yenye namba za usajili **T242EAX,** CHASSIS NAMBA **NZE1213307620,** ENGINE NAMBA **INZB638616** yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/1436/2025**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TUNDURU**

**Kituo cha MUNGOTI, Mkoa wa RUVUMA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na 180/ 2024**

**Jina la Mdai STILIO C/O MALITIN KAVINDI**

**Jina la Mdaiwa MOHAMEDI JANA MTILA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(kanuni ya 62 ya kanuni za Uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**

**KWA: MOHAMEDI JANA MTILA**

KWAMBA Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya Utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 27 mwezi 12 Mwaka 2024 kueleza kwanini Hukumu usitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo **20 mwezi 12 mwaka 2024**

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 32670 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late ELISHA GEORGE IBENGWE**

**And**

**In the Matter of Application for letters of administration by JOSHUA KULWA IBENGWE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 29 day of 01, 2025
Date at DAR ES SALAAM this 06 day of 01, 2025

Principal Resident Magistrate

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 31618 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JOSHUA MARTIN MWAKIBINGA........DECEASED**

**AND**

**In the matter of Application for letters of Administration by: -**

**JUDITH SIMON MWAIJANDE...................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (Rule 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20th day of January, 2025
Dated at Kyela, this 16th day of December, 2024

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE I/C
KYELA.

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 31758 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE TULIVANE FESTO KILAGANE ........DECEASED**

**AND**

**In the matter of Application for letters of Administration by: - JOSEPH ANYAMBALILE MWASUBILA................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (Rule 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 14th day of January, 2025
Dated at Kyela, this 17th day of December, 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Vikosi vya Russia, Ukraine vyakabiliana vikali Kursk

**KYIV, Ukraine**

ENEO la Kursk, limegeuka uwanja wa mapambano makali kati ya vikosi vya Russia na Ukraine.

Kursk eneo la Russia ambalo jeshi la Ukraine limeingia na kudhibiti sehemu ya ardhi, iliripotiwa mapigano makali katika saa 24 yaliyopita.

Kwa mujibu wa mkuu wa majeshi ya Ukraine, kulitokea makabiliano 218 kwenye maeneo yote ya mstari wa mbele ndani ya kipindi hicho.

Kupitia ukurasa wake wa Facebook, kamandi ya kikosi maalum cha Ukraine ilichapisha taarifa kwamba wanajeshi 13 wa Korea Kaskazini waliuawa, ingawa shirika la habari la Ujerumani DPA lilishindwa kuthibitisha taarifa hiyo kupitia vyanzo huru.

Mwishoni mwa wiki, Ukraine ilianzisha tena mapigano ya kushtukiza kwenye mkoa huo ulio magharibi mwa Russia na kwa mujibu wa Taasisi ya Utafiti wa Vita ya Marekani (ISW), vikosi vya Ukraine vimesonga mbele kuelekea kaskazini mashariki mwa mji wa Sudzha.

ISW ilisema hatua hiyo inaashiria kuwapo kwa operesheni iliyopangwa kwenye mkoa huo na pia matayarisho ya mashambulizi kwenye maeneo mengine ya mstari wa mbele.

Wizara ya Ulinzi ya Russia, katika taarifa yake ilikiri kwamba vikosi vyake vilikuwa vikikabiliana wanajeshi wa Ukraine kwenye maeneo kadhaa ya mkoa wa Kursk.

Kwa mara ya kwanza, vikosi vya Ukraine vilivuka mpaka wa nchi hizo mbili mwezi Agosti mwaka jana na tangu wakati huo vimeukalia mkoa wa Kursk, lakini kufuatia miezi kadhaa ya mapigano jeshi la Urusi limerejesha takribani nusu ya eneo hilo.

Katika kuhakikisha eneo hilo linabaki salama, Russia ilikubaliana na Korea Kaskazini kuwapeleka wanajeshi wa nchi hiyo kusaidia vikosi vyake kwenye mkoa huo.

***DW***



Waasi wa M23 wakiwa katika eneo la mapigano Mashariki mwa DRC hivi karibuni. **PICHA: AP**

# Jimmy Carter kuzikwa leo

**WASHINGTON, Marekani**

MAZISHI ya rais wa zamani wa Marekani, Jimmy Cater, yanafanyika leo nyumbani kwake katika jimbo la Georgia.

Kabla ya mazishi hayo, jeneza la mwili wa Carter, likiwa limefunikwa kwa bendera, liliwekwa katika jengo la bunge la Marekani la Capitol katika mji wa Washington DC, kwa siku mbili kwa ajili ya watu kupata nafasi ya kuaga.

Baada ya hapo ilifanyika ibada ya mazishi katika Kanisa Kuu la Katoliki la Washington.

Carter alifariki tarehe 29 mwezi Desemba akiwa na umri wa miaka 100 nyumbani kwake Georgia.

Awali shughuli za mazishi zilifanyika mjini Atlanta Jumamosi iliyopita katika Kituo cha Rais Carter, na kuruhusu mamia ya watu kumuaga kiongozi huyo.

Carter wakati wa uhai wake alishinda tuzo ya Nobel ya Amani, mkulima wa karanga, gavana wa Georgia na baadaye kukalia kiti cha urais wa Marekani baada ya kushinda uchaguzi wa 1976.

Hata hivyo, alikaa madarakani kwa muhula mmoja, akishindwa na Gavana wa zamani wa California, Ronald Reagan, mwaka 1980.

***BBC***

# Rwanda yataka ukweli wa DRC, isibebeshwe mzigo

**KIGALI, Rwanda**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Rwanda, Olivier Nduhungirehe, amekosoa jumuiya ya kimataifa kwa kushindwa kushughulikia chanzo cha mgogoro unaoendelea mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, badala yake inaisingizia kuwa chanzo.

Katika taarifa yake kupitia mtandao wa kijamii wa X, Nduhungirehe, aliwatuhumu waigizaji wa kimataifa kwa kukimbilia kulaani kundi la waasi wa M23, lililoteka eneo la Masisi hivi karibuni bila kuzingatia ukweli.

"Matamshi yao yanaishutumu Rwanda kwa mara nyingine tena kwa kuunga mkono M23 kwa kauli za upendeleo, ikitaja ukiukwaji wa mamlaka na uadilifu wa eneo la DRC," alisema.

Nduhungirehe alieleza mamluki wa Ulaya wamepelekwa eneo hilo kwa madai ya kuunga mkono jeshi la DRC kinyume na sheria za kimataifa na kukosoa EU kwa kukaa kimya na kutoshiriki katika shughuli za uhalifu zinazofanywa mamluki hao.

Waziri huyo aliongeza kuwa hakuna hata mmoja aliyetoa wito wa kufanyika mazungumzo ya moja kwa moja kati ya DR Congo na M23 ili kushughulikia chanzo cha mgogoro huo.

***BBC***

**"Matamshi yao yanaishutumu Rwanda kwa mara nyingine tena kwa kuunga mkono M23 kwa kauli za upendeleo, ikitaja ukiukwaji wa mamlaka na uadilifu wa eneo la DRC," alisema.**

# Kiongozi RSF awekewa vikwazo

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imemwekea vikwazo mkuu wa kundi la RSF nchini Sudan, Mohamed Hamdan Dagalo, baada ya kubaini vikosi vyake vinavyopigana Sudan kuhusika na mauaji ya kimbari.

Mapigano kati ya wanamgambo wa RSF na jeshi la Sudan yamesababisha mauaji ya maelfu ya watu na wengine mamilioni kukimbia nchi hiyo.

Vikwazo hivyo vinawalenga kumzuia kamanda huyo wa RSF na familia yake kusafiri kwenda Marekani na kufungia mali zao.

Hatua hiyo ni pigo kwa RSF ambayo inaijaribu kupanua himaya yake kwa kudhibiti nusu ya nchi hiyo.

Hata hivyo, RSF ilikanusha kuhusika uhalifu wa kivita na kueleza wanaofanya vitendo hivyo ni watu wasiotoka ndani ya kundi hilo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alisema katika taarifa yake kuwa RSF na washiriki wake wameendelea kushambulia raia.

Aliongeza kuwa walikuwa wakiua wazee na vijana wa kiume kwa msingi ya kikabila.

Pia walihusika na vitendo vya ubakaji kwa wanawake na aina nyingine za unyanyasaji wa kijinsia.

Marekani awali iliwahi kuweka vikwazo dhidi ya viongozi wengine, pamoja na maofisa wa jeshi, lakini haikuweka vikwazo dhidi ya Dagalo.

"Kwa kuwa ni kamanda mkuu wa RSF, Hemedti anawajibika kwa vitendo viovu na haramu vya vikosi vyake," ilisema Idara ya Hazina ya Marekani.

Marekani pia ilipiga vikwazo kampuni saba za RSF zilizoko UAE zinazohusishwa na kununua silaha.

***BBC***

HABARIMICHEZO

# KAGOMA: NAFUATA MAELEKEZO YA KOCHA

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Simba, Yusuph Kagoma, amesema amekuwa akifuata zaidi maelekezo ya kocha wake Fadlu Davids na ndio sababu ya kufanya vizuri kwenye michezo mbalimbali anayopewa nafasi ya kucheza.

Kagoma aliyesajiliwa na Simba kutoka Singida Black Stars mwanzoni mwa msimu huu amekuwa na kiwango kizuri huku Kocha Fadlu akimtumia mara kwa mara.

Akizungumza na Nipashe, Kagoma, alisema anashukuru kupata nafasi kwenye kikosi cha Simba lakini kazi yake inaonekana bora kutokana na kufuata kile kocha wake anachomtuma kwenda kukifanya.

"Simba ina wachezaji wazuri na wenye ubora, si kazi nyepesi kupata nafasi ya kucheza, lakini nashukuru kila nikipata nafasi naenda kufanya kile mwalimu anachoniagiza kwenda kukifanya," alisema Kagoma.

Akizungumzia michezo iliyobakia ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kagoma alisema hakuna mchezo mwepesi kati iliyobakia na lazima wapambane ili waweze kujihakikishia kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Simba imebakisha michezo dhidi ya Bravo do Maquiz watakaocheza ugenini Januari 12 nchini Angola na mchezo dhidi ya CS Costantine watakaocheza kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, Januari 19.

"Hakuna mchezo mwepesi hapo, kila mchezo tunatakiwa kupambana kupata alama tatu, kwa sasa akili zetu zipo kwenye mchezo dhidi ya Bravo, ni lazima tukapambane kupata ushindi, na inawezekana," alisema Kagoma.

Simba inashika nafasi ya pili kwenye kundi lake ikiwa na pointi tisa sawa na vinara CS Costantine lakini wakiwa juu kutokana na uwiano wa mabao ya kufunga na kufungwa, Bravo wanashika nafasi ya tatu wakiwa na pointi sita huku CS Sfaxien wakiburuza mkia kwa kutokuwa na pointi.



Winga wa Kilimanjaro Stars, Iddi Suleiman 'Nado' (kulia), akijaribu kumtoka beki wa timu ya taifa ya Kenya kwenye mchezo wa Kombe la Mapinduzi uliochezwa juzi usiku Pemba, Kenya ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Mkazi Tanga aibuka kidedea

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Horohoro Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, Athuman Mrisho, ameibuka mshindi wa shilingi milioni 10 katika shindano la 'Magifti'.

Kampuni ya Yas ilimtangaza mshindi huyo katika droo ya saba ya shindano hilo.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Mrisho, alisema fedha hizo alizozipata zinaenda kubadilisha maisha yake kwa kuwa atawekeza kwenye biashara zaidi.

"Kwa kweli nashukuru sana kwa ushindi huu, fedha hizi zitanisaidia sana kwenye biashara zangu, zinakwenda kunibadilishia maisha yangu, nawashukuru sana Yas kwa kuendesha shindano hili," alisema Mrisho.

Kwa upande wake, Meneja wa kampuni hiyo Mkoa wa Tanga, Amani Sailoja, amempongeza mshindi huyo ambapo mbali na mambo mengine amesema fedha hizo akizitumia vizuri zitamwinua kiuchumi.

**"Nitoe wito kwa wananchi kushiriki katika kampeni hizi tunazozitoa, nim pongeze mshindi kwa kufanikiwa kupata fedha hizi ambazo naamini zi tamsaidia katika shughuli zake," alisema Sailoja. Kampuni hiyo imetumia shilingi milioni 250 katika kampeni hiyo kurudisha kwa jamii kile wanachoki pata.**

# Kagera Sugar yamfuata Nkane Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kagera Sugar imetajwa ipo kwenye mazungumzo na klabu ya Yanga kwa ajili ya uwezekano wa kumpata winga wa timu hiyo, Denis Nkane.

Habari kutoka ndani ya klabu ya Kagera Sugar zinasema kuwa uongozi huo umepiga hodi Yanga kumtaka mchezaji huyo kwa mkopo wa miezi sita wakiwa na imani kuwa anaweza kuwasaidia kwenye mechi za mzunguko wa pili.

"Tunajua ni mchezaji mzuri, ni winga mwenye kasi na kipaji, ila Yanga kuna wachezaji wakubwa na maarufu ndiyo maana hapati nafasi ya kucheza. Tunajua kuwa alianza kuchezeshwa na Kocha Miguel Gamondi, tumejidhihirisha kuwa bado ana kiwango kizuri licha ya kwamba kuna wakati alikuwa anachezesha sehemu ambayo hajaizoea, lakini sisi tunamtaka atusaidie kama winga ili tuongezea ubora kwenye kikosi chetu, nadhani tutafanikiwa kwa hilo kwa sababu mipango inakwenda vizuri," alisema mtoa taarifa ndani ya klabu hiyo.

Kagera Sugar haijawa na mwanzo mzuri hadi katikati ya ligi ikiwa inashika nafasi ya 15 ambapo katika michezo 15 iliyocheza imeambulia pointi 11 tu, ikishinda michezo miwili, sare tano na kupoteza minane.

Katika kujizatiti kutaka kuboresha kikosi hicho, imeelezwa Kocha Mkuu, Melis Medo pia anamuhitaji kinara wa ufungaji kwenye Ligi ya Championshio, Raizin Hafidh kutoka Mtibwa Sugar.

Medo ambaye aliifundisha Mtibwa kwenye michezo ya mwanzo ya ligi hiyo kabla ya kunyakuliwa na Kagera Sugar, anamuhitaji Raizin ambaye mpaka sasa amepachika mabao 11 akiiwezesha timu hiyo yenye maskani yake Turiani, Morogoro kuongoza ligi hiyo.

## ZISIKUPITE

### KLABU TATU ZAMTAKA RASHFORD

KLABU za Borussia Dortmund na Juventus zimejiunga na AC Milan katika mbio za kumnunua mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27. ***(Sky Sports)***

### MARMOUSH AWANIWA MAN CITY

KLABU ya Manchester City inavutiwa na dili la kumsajili mshambuliaji wa Misri, Omar Marmoush mwenye umri wa miaka 25 anayeichezea Eintracht Frankfurt, ambaye thamani yake inakadiriwa kuwa euro milioni 50. ***(Espn)***

### MURILLO NA FOREST MAMBO SAFI

KLABU ya Nottingham Forest inajadili mpango wa kuongeza mkataba wa beki wa Brazil, Murillo mwenye umri wa miaka 22, ambao kwa sasa unamalizika 2028. ***(Athletic)***

### PEREIRA ATAKIWA PALMEIRAS

KLABU ya Palmeiras ina nia ya kumsajili kiungo mshambuliaji wa Brazil, Andreas Pereira mwenye umri wa miaka 29, lakini bado hawajakubaliana na Fulham. ***(Fabrizio Romano)***

### KERKEZ ATAKIWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili beki wa Hungary, Milos Kerkez lakini bei ya pauni milioni 40 ya Bournemouth kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 inaweza kuwa kikwazo. ***(Team Talk)***

### CAENEY CHUKWUEMEKA AFUATILIWA

KLABU ya Borussia Dortmund inamfuatilia kiungo mshambuliaji wa Chelsea mwenye umri wa miaka 21, Carney Chukwuemeka. ***(Sky Germany)***

### ARSENAL YAMTAKA NICO WILLIAMS

ARSENAL inavutiwa na winga wa Athletic Bilbao, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22, lakini hawataweza kumnunua raia huyo wa Hispania mwezi huu kwa sababu ya matatizo ya kifedha. ***(Talksport)***

### S'HAMTON KUMUUZA WALKER-PETERS

KLABU ya Southampton inatarajia kumuuza beki wa England, Kyle Walker-Peters mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake unaisha msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### HAWAJAPOKEA OFA KUIUZA LIVERPOOL

WAMILIKI wa Liverpool, Fenway Sports Group, hawajapokea ombi kutoka kwa mnunuzi yeyote wa klabu hiyo baada ya baba yake Elon Musk, Errol kusema kuwa mwanawe ana nia ya kuwanunua majogoo hao wa Anfield. ***(Sky Sports)***

### PSG KUMSAJILI JHON DURAN

PSG wana nia ya kumsajili Jhon Duran na inaaminika Aston Villa wanaweza kushawishika kumuuza mshambuliaji huyo wa Colombia mwenye miaka 21 kwa ada ya Euro milioni 60. ***(Sportsport)***

### BARCERONA NAO WAMTAKA

Mkurugenzi wa michezo wa Barcelona, Deco amekutana na wawakilishi wa Duran kwa mazungumzo yasiyo rasmi ili kumjulisha mshambuliaji huyo wa Aston Villa kuwa yuko kwenye rada za klabu hiyo ya Catalan. ***(Sport - kwa Kihispania)***

### BAYERN KUIVURUGIA MAN UNITED

Bayern Munich wanataka kuvuruga ombi la Manchester United la kutaka kumsajili mshambuliaji wa Uswisi, Viktor Gyokeres mwenye miaka 26 kutoka Sporting. ***(Star)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MAINOO KWENYE RADA ZA CHELSEA

●●●Klabu hiyo inaongoza mbio za kumsajili nyota huyo huku wakisubiri kama...

**LONDON, England**

CHELSEA imeripotiwa kuongoza katika mbio za kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United, Kobbie Mainoo iwapo hataongeza mkataba wake Old Trafford.

Mainoo mwenye miaka 19 alitia wino mkataba wa miaka minne mwaka 2023, muda mfupi kabla ya kuanza kucheza Ligi Kuu ya England, na anadaiwa kuwa mchezaji anayelipwa mshahara wa chini zaidi katika kikosi cha wakubwa ambapo anachukua pauni 20,000 kwa wiki.

Licha ya nia ya United ya kutaka kumwongezea muda na kumtambua kiungo huyo kama mchezaji muhimu wa kikosi cha kwanza, maendeleo ya mazungumzo kuhusu masharti mapya yamekuwa ya polepole na sasa kuna wasiwasi kuhusu mustakabali wa muda mrefu wa Mainoo ndani ya United.

Gazeti la Daily Mail, limeandika Chelsea wamejiweka mbele ya foleni ya kuwania saini ya Mainoo, wakimwona kijana huyo kama nyota ajaye.

Hapo awali ilidaiwa kuwa Mainoo alikuwa sehemu ya kundi dogo la wachezaji ambao United iliwaona kama ‚wasioguswa', ingawa David Ornstein wa The Athletic hivi karibuni aliandika kwamba haikuwa hivyo kwa sababu ya faida halisi ambayo inaweza kupatikana kwa kumuuza mhitimu huyo wa akademi yao.

"Ikiwa kuondoka kutatokea kwa Marcus Rashford, kuna uwezekano mkubwa wa kuuzwa wachezaji zaidi msimu wa joto," aliandika Ornstein.

"Kwa jinsi Kobbie Mainoo anavyoweza kuwa, mkataba wake unamalizika 2027, hakuna habari juu ya mkataba mpya.

"Alejandro Garnacho pia, sidhani kama kuna mtu yeyote kwenye mabano hayo hayupo kwenye meza. Ni nani, ni mtu kama Leny Yoro, kama Amad Diallo nadhani hawawezi kuguswa."

Muhimu zaidi, wakati mkataba wa Mainoo unaendelea hadi 2027, United wana chaguo la kuongeza muda huo kwa miezi 12 zaidi, na kuwaacha na shinikizo dogo sana la haraka kufanya uamuzi juu ya mustakabali wa Mwingereza huyo.

## HABARI MICHEZO

## Deschamps kuiacha Ufaransa baada Kombe la Dunia 2026

**PARIS, Ufaransa**

DIDIER Deschamps ataacha jukumu lake kama kocha mkuu wa Ufaransa mwishoni mwa mkataba wake wa sasa unaofikia kilele baada ya Kombe la Dunia la 2026, kwa mujibu wa ESPN.

Mshindi wa Kombe la Dunia 2018 ataondoka baada ya Kombe la Dunia nchini Marekani, Canada na Mexico ikiwa Les Bleus itafuzu, au ataondoka baada ya kumalizika kwa kampeni za kufuzu ikiwa watashindwa.

Zinedine Zidane mwenye umri wa miaka 52, kocha wa zamani wa Real Madrid, mshindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo na mchezaji mwenzake wa zamani na Deschamps kwenye timu ya Ufaransa, ndiye anayepewa nafasi kubwa kuchukua nafasi yake.

Deschamps mwenye miaka 56, alichukua mikoba ya Laurent Blanc miaka 14 iliyopita kwenye benchi ya Ufaransa msimu wa majira ya joto wa 2012 na kuleta mafanikio ambayo hayajawahi kushuhudiwa kwa timu ya taifa.

Pamoja na kushinda Kombe la Dunia la 2018 na Ligi ya Mataifa ya Ulaya 2021, alifika fainali za Euro 2016 na Kombe la Dunia 2022 na nusu fainali ya Euro 2024.

Yeye ndiye kocha mkuu wa Ufaransa aliyefanikiwa zaidi kuwahi kutokea, akiwa na asilimia 64.2 ya ushindi na kufika angalau nusu fainali katika michuano minne mikubwa iliyopita.

Pia ni mmoja wa makocha wa timu ya taifa waliokaa muda mrefu na wenye mafanikio makubwa katika historia. Yeye ni mtu wa tatu pekee kushinda Kombe la Dunia akiwa mchezaji (mwaka 1998) na kocha akiungana na Mjerumani Franz Beckenbauer na Mbrazili Mario Zagallo.

Ufaransa itatafuta nafasi ya kundi lao la kufuzu baada ya kumaliza mashindano ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya ambayo yanaanza kwa mechi ya robo fainali dhidi ya Croatia Machi.

## Endrick atakiwa kuwa na subira Real Madrid

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid imemtaka Endrick kuwa mvumilivu huku mshambuliaji huyo chipukizi akipendekezwa kuchelewesha uamuzi wowote kuhusu mustakabali wake na klabu hiyo hadi majira ya kiangazi baada ya kuanza vibaya soka la ulaya.

Endrick alisajiliwa na Madrid kwa dili la euro milioni 60 wakati akiwa kijana mwenye umri wa miaka 16 kutoka Brazil, alihamia kwa miamba hao wa Hispania alipofikisha umri wa miaka 18 msimu uliopita wa joto, lakini ameona ni vigumu kupata muda wa kucheza huku kukiwa na ushindani kutoka kwa Vinicius Junior, Rodrygo na Kylian Mbappe.

Uwepo wa Brahim Diaz na Arda Guler pia unaongeza ushindani kwake, na kusababisha uvumi wa yeye kutaka kuhama kutoka mji mkuu wa Hispania, Madrida.

Endrick amecheza mechi 16 sawa na jumla ya dakika 250 na hajafunga bao tangu Septemba 17 mwaka jana. Alianza mechi ya Madrid ya Copa del Rey dhidi ya Minera ya daraja la nne Jumatatu usiku katika kile kilichotajwa kuwa "nafasi yake ya mwisho".

Hata hivyo, licha ya ushindi wa Madrid wa mabao 5-0, Endrick hakuwa miongoni mwa wafungaji.

The Athletic limeandika kuwa Madrid wamemtaka Endrick, ambaye alifunga mabao ya kimataifa dhidi ya England na Hispania msimu uliopita akiwa bado mchezaji wa Palmeiras kuwa na subira.

Vinicius Junior na Rodrygo vile vile walifanya mipango iliyopangwa mapema wakiwa na umri mdogo na hawakuwa nyota wa haraka, huku Endrick akionekana katika michezo mingi kufikia sasa kuliko walivyofanya nyota hao katika msimu wao wa kwanza.

Endrick hana mpango wa kuondoka Bernabeu wakati wa usajili wa Januari hii, lakini anatarajiwa kushughulikia hali hiyo mwishoni mwa msimu ikiwa mambo hayatakuwa sawa.



## ARTETA ASINGIZIA MPIRA KIPIGO KWA NEWCASTLE

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amesema kushindwa kwa Arsenal kuuzoea mpira wa Kombe la Carabao kulichangia kupata kichapo cha mabao 2-0 katika mchezo wa kwanza wa nusu fainali dhidi ya Newcastle United juzi Jumanne.

Mabao kutoka kwa Alexander Isak na Anthony Gordon yaliwaweka vijana wa Eddie Howe katika nafasi ya uongozi kabla ya mechi ya marudiano Februari 5.

Washikabunduki hao walipoteza nafasi nyingi za kufunga mabao na wakamaliza mchezo huo kwa kichapo hicho.

Alipoulizwa angeweza kufanya nini ili kuepuka nafasi alizokosa kuwa tatizo la kisaikolojia, Arteta alirejelea mabadiliko ya mpira kulingana na kanuni za mashindano na toleo la Puma lililotumika badala ya mpira wa kawaida wa Nike.

"Jaribu tu kuwaonesha, wape vidokezo vya kile tunaweza kufanya vizuri zaidi," alisema Arteta.

"Nadhani tulipiga mipira mingi juu ya lango na mpira huu unaruka sana. Tunajadili hilo pia, kuna maelezo ambayo tunaweza kufanya vizuri zaidi. Lakini lazima hilo liishe katika mchezo ujao.

Akisisitiza juu ya suala la mpira, Arteta aliendelea, "Ni tofauti tu, tofauti sana na mpira wa Ligi Kuu na unapaswa kuzoea hilo kwa sababu unaruka tofauti. Unapougusa, mshiko ni tofauti sana na lazima tubadilike na tuzoee."

Arteta alikuwa sehemu ya makocha Manchester City wakati Pep Guardiola alipolalamika kuhusu mpira huo baada ya mechi ya raundi ya nne Oktoba 2017. Guardiola alidai "kufunga na mpira huo ni muujiza", kwani mpira wa Miter (Puma) una kasi yake.

Baadaye EFL ilitoa taarifa iliyosomeka: "Mpira wa Miter uliotumika katika Kombe la Carabao msimu huu una sifa ya kiufundi sawa na mipira yote ilijaribiwa kwa mujibu wa ubora wa FIFA.

"Mipira yote inayotumika katika mchezo wa kulipwa inatakiwa kufikia kiwango cha juu."

HABARI MICHEZO

# MZIZE AFUNGUKA MIPANGO KUCHEZA SOKA KIMATAIFA

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI akijipanga kuisaidia timu yake kutinga hatua ya robo fainali katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize, amesema anafurahi kuona jina lake linatajwa na klabu mbalimbali za nje ya Tanzania.

Mzize ambaye alionyesha kiwango kikubwa na kufunga mabao mawili katika ushindi wa magoli 3-1 dhidi ya TP Mazembe kutoka DR Congo, mechi iliyochezwa Januari 4, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, alisema anaamini muda ukifika kila kitu kitawekwa hadharani.

Mzize alisema anaamini bado mchango wake unahitajika kwa sasa ndani ya Yanga na akili yake yote ni kuona wanafanya vizuri katika mashindano ya kimataifa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nyota huyo alisema anajisikia furaha kubwa kuona wanaendelea Yanga inapata mwendelezo wa matokeo chanya katika kwenye mechi za kimataifa kwa sababu wanahitaji kufikia malengo ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ya CAF (Shirikisho la Soka Afrika).

Aliongeza Mzize amesema kuwa walikuwa wanahitaji kupata ushindi kwenye mchezo wao dhidi ya TP Mazembe jambo ambalo liliwezekana licha ya ushindani kuwa mkubwa kwenye mchezo huo.

"Ilikuwa ni muhimu kwetu kupata matokeo mazuri licha ya ushindani ambao upo katika hatua hii, tunaamini tutazidi kupambana katika mechi zinazofuata ili tufikie malengo yetu, hakuna mechi rahisi katika hatua ya makundi, kila timu ina ubora," alisema Mzize.

Tayari Al Hilal ya Sudan yenye pointi 10 tayari imeshatinga hatua ya robo fainali wakati MC Alger iko katika nafasi ya pili na pointi zake tano, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanafuata wakiwa na pointi nne na TP Mazembe yenye pointi mbili inaburuza mkia.

Yanga imebakiza mechi moja nyumbani dhidi ya MC Alger kutoka Algeria na itasafiri kuifuata Al Hilal ambayo inacheza mechi zake mjini Lubumbashi, DR Congo.




Nahodha wa Timu ya vijana ya umri chini ya miaka 15 ya JKT Queens, Lydia Kabambo (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Kenya Academy Sports katika mechi ya mashindano ya Wasichana ya CAF U-15 (GIFT 2025), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi. JKT Queens ilipata ushindi wa mabao 3-0. **PICHA: TFF**

# Kili Stars kukamilisha ratiba

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Soka ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), inatarajia kuwakabili Burkina Faso katika mechi ya kukamilisha ratiba ya mashindano ya kuwania Kombe la Mapinduzi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Gombani ulioko Kisiwani Pemba.

Kilimanjaro Stars tayari imeshaondolewa katika mashindano hayo baada ya kukubali kichapo cha pili mfululizo katika michuano hiyo ambayo mwaka huu inashirikisha timu za taifa.

Ushindi wa mabao 2-0 waliopata Kenya katika mechi iliyochezwa juzi usiku ilimaliza ndoto za Kilimanjaro Stars kuendelea katika michuano hiyo.

Katika mechi ya kwanza ya ufunguzi, Kilimanjaro Stars inayonolewa na Kocha Mkuu, Hamad Ally, ilifungwa bao 1-0 na wenyeji, Zanzibar (Zanzibar Heroes).

Mechi nyingine ya michuano hiyo ya kukamilisha hatua ya awali itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Zanzibar Heroes dhidi ya Burkina Faso.

Katika msimamo wa mashindano hayo, Kenya yenye pointi nne sawa na Burkina Faso iko kileleni ikifuatiwa na Zanzibar Heroes yenye pointi tatu.

Fainali ya mashindano hayo itafanyika Januari 13, mwaka huu kwa kushirikisha timu itakayomaliza katika nafasi ya kwanza dhidi ya nchi itakayokuwa iko kwenye nafasi ya pili.

## Simba : Ni safari kufunga hesabu

INATOKA UK. 24

Sisi kama wachezaji tuna ari kubwa na ile presha ya mwanzo imetuondoka, unajua mnavyozidi kucheza na kupata ushindi inawaondolea presha na kuwapa nguvu ya kujiamini," alisema beki huyo.

Wakati huo huo Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema katika dirisha dogo lililofunguliwa, klabu hiyo mpaka sasa imemsajili mchezaji mmoja tu ambaye ni Elie Mpanzu, huku akisema hawatasajili kwa fasheni.

Ahmed alisema hawatasajili mchezaji wa kujaza idadi au mchezaji wa kukaa benchi, bali wanahitaji nyota ambaye moja kwa moja anaingia katika kikosi cha kwanza.

"Hakuna mapungufu makubwa sana katika kikosi chetu, hao wengine wacha wakusanye wachezaji, sisi kama tutafanya usajili basi utakuwa wa mchezaji mmoja au wawili, na wawe wa viwango vya juu, hata wakija basi moja kwa moja wanaingia kwenye kikosi cha kwanza," alisema Ahmed.

Kimahesabu Simba yenye pointi tisa, inahitaji sare tu ili kusonga mbele, pointi ambazo hazitafikiwa na Bravo do Maquis au CS Sfaxien.

## Maxi 'out' Yanga ikiwafuata Al Hilal

INATOKA UK. 24

tayari kupambania nafasi yetu ya kucheza robo fainali," alisema Ramovic.

Aliongeza wachezaji wake wapo katika hali nzuri na shauku ya kuhakikisha wanafikia malengo kupitia mchezo huo muhimu.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema maandalizi kwa ajili ya safari ya leo yamekamilika ingawa wanasikitika kuwaacha nyota wake watatu.

"Wachezaji wengine wote wapo katika hali nzuri na wataondoka kwenda kusaka alama tatu muhimu zaidi kwetu, tunahitaji ushindi ili kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kucheza robo fainali, tunafahamu ugumu wa kundi letu lakini lazima tupambane mpaka mchezo mwisho," alisema Kamwe.

Yanga inashika nafasi ya tatu katika Kundi A ikiwa na pointi nne baada ya kucheza michezo minne, hivyo inahitaji ushindi ili kufufua matumaini ya kutinga robo fainali ambayo kwa sasa wanaonekana kuigombania na MC Alger yenye pointi tano wakiwa nafasi ya pili nyuma ya Al Hilal.

Licha ya kucheza nje ya nyumbani, vigogo hao wa Sudan, Al Hilal wanaofundishwa na Mkongomani, Florent Ibenge, tayari wameshafuzu hatua ya robo fainali baada ya kufikisha pointi 10.

Michezo
Alhamisi Januari 9, 2025
Nipashe

**Mainoo kwenye rada za Chelsea**
UKURASA 21



# Simba : Ni safari kufunga hesabu

## ●●●Fadlu afunguka ubora wa Mpanzu hautakamatika baada...

**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA kulala, tayari kikosi cha Simba kimeondoka nchini leo alfajiri kuelekea Angola ili kuifuata, Bravos do Maquis, kwa ajili ya mechi ya raundi ya tano ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa Jumapili mjini Luanda.

Katika mechi ya kwanza Simba yenye pointi tisa kibindoni kwa sasa, ikiwa mwenyeji, ilipata ushindi wa bao 1-0.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alisema kikosi chake kinaenda Angola kwa kazi moja ya kumaliza ‚kazi' ya kusaka pointi tatu muhimu ili kujihakikisha tiketi ya kucheza hatua inayofuata ya robo fainali.

Fadlu alisema kila mchezaji wa Simba yuko tayari kupambana ili kufikia malengo na anaamini msimu huu watapata mafanikio katika mashindano yote wanayoshiriki.

Kocha huyo pia amemtetea winga wake, Ellie Mpanzu, ambaye mechi iliyopita ugenini dhidi ya CS Sfaxien, alionyesha kiwango kizuri, alisema bado hajawa fiti na utimamu wa mwili wa kucheza dakika zote 90.

Alisema wanatarajia mengi kutoka kwa winga huyo ambaye kwa sasa hana utimamu wa mwili kamili, ndiyo maana amekuwa akimfanyia mabadiliko katika kila mechi aliyocheza.

"Ana wiki tatu tu tangu aanze kucheza mechi za ushindani, nimekuwa nikimpa dakika kadhaa za kucheza, mimi hapa nina furaha sana kwa kile anachokionyesha ndani ya uwanja, kiufundi amekuwa na athari chanya kwa wapinzani wetu kwa jicho la kitaalamu, huwezi kuliona hilo kama si mwalimu, mpira una vitu vingi zaidi ya ‚asisti' na mabao uwanjani.

Ili upate hivyo kuna mchakato unafanyika ndani, amekuwa akifanya kazi kwa usahihi na kufuata maelekezo, tatizo hajawa na pumzi na utimamu wa mwili wa kumaliza dakika 90 akiwa na ubora ule ule," Fadlu alisema.

Aliongeza taratibu anaanza kuwa fiti, na kila mechi atakuwa akimwongezea muda mpaka atakapoweza kumaliza dakika zote 90.

"Najua akishakuwa na uwezo wa kucheza dakika 90, atakuwa hatari zaidi ya hivi alivyo, uzuri sisi tunamfahamu, tunafahamu kipaji chake na uwezo wake mkubwa, hivyo haitupi wasiwasi tunajua atafanya makubwa tu," alisema kocha huyo.

Naye nahodha wa Simba, Mohamed Hussein ‚Zimbwe Jr', alisema wanakwenda kupambana kusaka ushindi au sare, matokeo ambayo yataiwezesha timu yao kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo kutoka Kundi A.

"Mchezo utakuwa mgumu kwa sababu wenzetu wametoka kupoteza dhidi ya CS Constantine, nao jicho lao litakuwa katika mchezo huo, kama wachezaji tutakwenda kupambana kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, matumaini yetu ni kupata matokeo mawili, ushindi au sare, tukifanikiwa hapo tutakuwa tumefuzu tayari.

INAENDELEA UK. 23



Winga wa kimataifa wa Simba kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), Ellie Mpanzu (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa CS Sfaxien katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyochezwa Jumapili iliyopita jijini Tunis, Tunisia. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Maxi 'out' Yanga SC ikiwafuata Al Hilal

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI kikosi cha Yanga kinatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Mauritania kuifuata Al Hilal kwa ajili ya mechi ya raundi ya tano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kiungo nyota, Maxi Nzengeli, hatakuwa sehemu ya mchezo huo.

Mbali na Nzengeli, Yaou Kouassi na Aziz Andambwile, pia wanabakia nchini kutokana na kutokuwa fiti kuwakabili vinara hao wa Kundi A.

Al Hilal itaikaribisha Yanga katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Jumapili kuanzia saa 4:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa Novemba 26, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga walikubali kipigo cha mabao 2-0.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, alisema mchezo huo ni muhimu zaidi kwao katika mbio zao za kusaka tiketi ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Ramovic alisema wanakwenda Mauritania wakitambua wanatakiwa kupata ushindi kwa sababu wanafahamu wakipoteza mchezo huo watakuwa wamejiweka katika hali ngumu kwenye mbio za kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Ni mchezo tunaohitaji zaidi ushindi, hautakuwa mchezo mwepesi lakini tumejiandaa vizuri, kikubwa kila mchezaji anafahamu sehemu tulipo na nini tunatakiwa kufanya, tupo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042